Nipashe
Jumatano Desemba 23, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580438
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Msimamizi** mizani jela miaka mitatu kwa rushwa
UKURASA 3



**Mbaroni** tuhuma mauaji ya mke kisa wivu mapenzi
UKURASA 3



Laporta: Nataka Messi abaki Barca
UKURASA 20

# Polisi, mfanyabiashara mbaroni madai utapeli

UKURASA 2



Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Shariff Hamad, akizungumza na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, ofisini kwake visiwani Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Ummy, Mwinyi, Maalim wateta Zanzibar

UKURASA 2



## Waziri kuyashughulikia mabasi uvunjaji sheria

UKURASA 2

**MICHEZO** **SVEN: BOCCO, MANULA 'OUT', HAKUNA NAMNA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Polisi, mfanyabiashara tanzanite mbaroni kwa tuhuma za utapeli

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani Arusha, linamshikilia mfanyabiashara wa madini ya tanzanite na askari polisi wanne, kwa tuhuma za kujipatia Sh. milioni 15 kwa njia ya utapeli, ili kumsaidia kigogo mmoja wa madini hayo kukwepa mtego wa kesi inayohusiana na uhujumu uchumi.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Kamishna Msaidizi Salum Hamduni, alithibitisha jana kukamatwa kwa mfanyabiashara huyo pamoja na askari hao wanaodaiwa kutokea mkoani Dodoma.

"Ni kweli tunawashikilia polisi wanne na mfanyabiashara huyo, ila bado tuko katika uchunguzi na ukikamilika tutatoa taarifa rasmi na watuhumiwa watafikishwa mahakamani baada ya uchunguzi kukamilika," alisema.

Inadaiwa kuwa askari hao walipewa dili na mfanyabiashara huyo wa tanzanite kwenda ofisini kwa mfanyabiashara maarufu wa madini ya tanzanite ambaye ni kiongozi wa Chama cha Wauzaji Madini Tanzania (TAMIDA) kujitambulisha kuwa wao ni maofisa kutoka kikosi maalum makao makuu.

Baada ya maofisa hao wa polisi kufika eneo hilo, kigogo huyo wa TAMIDA (jina linahifadhiwa) alikamatwa na polisi hao waliojitambulisha kutoka kikosi maalumu na kutaka wapewe Sh. milioni 30, ili wamwachie kwa vile anatuhumiwa kukwepa kodi na anakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi.

Baada ya maelezo hayo na kumkamata, inadaiwa kuwa maofisa hao wanne wa polisi waliondoka na kiongozi huyo wa TAMIDA na kwenda naye hadi eneo la Makuyuni na kupatiwa kiasi cha Sh. milioni 15 kati ya Sh. milioni 30 walizotaka.

Inadaiwa kuwa baada ya kufanikiwa kupata kiasi hicho cha fedha, maofisa hao wa polisi walifuata mgao mwingine wa Sh. milioni 15 Jumatatu ya wiki iliyopita ambazo zilizobakia, lakini kiongozi huyo wa TAMIDA alikuwa tayari ameweka mtego kwa kushirikiana na makachero wa Jeshi la Polisi.



Balozi wa Indonesia nchini, Ratlan Pardede (kulia), akisisitiza jambo kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela (kushoto), alipomtembelea jana ofisini kwake, kuzungumza namna ya kushirikiana kwenye uwekezaji hususani sekta ya kilimo hasa viungo, matunda, mboga, madini na utalii. Wapili kushoto ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Judica Omari. **PICHA: OSCAR KASIMIRI**

## Ummy ateta na Mwinyi, Maalim Seif Zanzibar

**Na Lulu Mussa,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, jana alifanya ziara ya kikazi visiwani Zanzibar kwa lengo la kujitambulisha.

Katika ziara hiyo, Ummy alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Ikulu Zanzibar.

Katika mazungumzo yao, Ummy alisema kuwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Zanzibar, amedhamiria kuendeleza jitihada za kutatua kero za Muungano zilizobakia.

"Mheshimiwa Rais, nikuhakikishie kuwa nitafanya kazi kwa karibu sana na Mheshimiwa Khalid, waziri mwenzangu kuhakikisha hoja ambazo bado hazijapatiwa ufumbuzi, zinafanyiwa kazi na mwanzoni mwa Januari tunategemea kuwa na kikao cha pamoja baina yetu," Ummy alisema.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Mwinyi, alimpongeza Ummy kwa kuteuliwa tena kuwa waziri na kusisitiza kuwa serikali yake itampa ushirikiano katika kuratibu masuala ya Muungano.

Katika hatua nyingine, Waziri Ummy alifanya mazungumzo na Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharrif Hamad Chukwani Zanzibar.

Katika mazungumzo yao, Maalim Seif alisisitiza umuhimu wa wizara zenye hoja za Muungano kukutana na kutafuta suluhu ya mapema na kuhamasisha wizara zisizo na hoja kukutana pia kwa lengo la kudumisha undugu baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

"Ninashauri na kusisitiza wizara zinazoshabihiana, zikutane na kuhakikisha hoja zinazopatiwa ufumbuzi zitekelezwe ipasavyo," alisema Maalimu Seif.

Waziri Ummy yuko visiwani Zanzibar kwa ziara ya kikazi ya siku mbili na leo anatarajiwa kutembelea miradi ya Muungano inayotekelezwa pande zote mbili.

# Simbachawene kuyashughulikia mabasi 16 kuvunja sheria

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ameyaonya mabasi 16 ya abiria yanayofanya safari zake mikoani kuacha mara moja tabia ya kuvunja sheria za usalama barabarani, zinazohatarisha maisha ya Watanzania wanaotumia huduma hizo.

Waziri Simbachawene, alitoa onyo hilo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari, jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa kuhusu hali ya usalama na matukio ya ajali za barabarani nchini hususan katika kipindi cha kuelekea Sikukuu za Krismas na Mwaka Mpya.

Mabasi yaliyoonywa ni pamoja na T367 ARH-Asante Rabbi yanayofanya safari zake za Arusha kuelekea Mwanza, T498 BYZ-Kidia One linalotoka Mwanza kuelekea Dar es Salaam, T395 BAP-Asante Rabbi (Arusha-Mwanza), T718 DPK-Maning Nice (Morogoro-Masasi), T695 DMJ-Ally's Star (Dar es Salaam-Mwanza), T424 AWB-Mgamba (Mwanza-Arusha), T253 DHM-Capricon (Arusha-Mbeya) na T400 AKM-Yellow line (Singida-Mbeya).

Mabasi mengine ni, T756 DNT-Ally's Star (Mwanza- Dar es Salaam), T260 DUC-Frester (Dar es Salaam- Mwanza), T221 DKB-Saratoga (Dar es Salaam-Kigoma), T988 AHB-Capricon, T450 AWJ-Frester, T774 DRL-BM (Arusha- Dar es Salaam), T768 DRL-BM (Arusha- Dar es Salaam), T775 DRL-BM (Arusha-Dar es Salaam).

Simbachawene, alisema hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa mabasi yote yanayokiuka Sheria za Usalama Barabarani. "Nimesema nitachukua hatua kali za kisheria kwa ajili ya mabasi yote niliyoyataja na yote yatakayobainika kuvunja sheria zote za usalama barabarani, na hili nalisema kwa uwazi kabisa madereva acheni kuhatarisha maisha ya Watanzania," alisema Simbachawene.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa chanzo kikubwa cha ajali za barabarani ni pamoja na makosa ya kibinadamu, ubovu wa vyombo, madereva kuendesha magari au vyombo vya moto kwa mwendo kasi kinyume cha sheria.

Vile vile, Simbachawene ameeleza hali ya usalama kwa kipindi cha Januari hadi Novemba, 2020 kuwa ni nzuri, uhalifu umedhibitiwa kwa kiwango kikubwa. "Pamoja na kuwapo kwa uhalifu wa makosa madogo yanayoendelea kujitokeza, Jeshi la Polisi nchini limefanikiwa kuyapunguza makosa hayo."

"Kwa upande wa usalama barabarani, takwimu za ajali barabarani kuanzia Januari, 2019 hadi Novemba, 2021 zinaonyesha idadi ya ajali, vifo na majeruhi zinaendelea kupungua," alisema Simbachawene.

Vilevile, ameeleza takwimu za mwaka 2020 zinaonyesha kuwa kuna upungufu wa ajali 921 ambayo ni asilimia 37, vifo 194 sawa na asilimia 14 na majeruhi 636 ambayo ni sawa na asilimia 24 kulinganisha na mwaka 2019.

Alitoa rai kwa wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kuzuia ajali za barabarani na kupambana na uhalifu kwa kutii sheria bila shuruti.

HABARI KITAIFA

# Msimamizi mizani jela kwa rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Chato Mkoa wa Geita imemhukumu Msimamizi Mkuu wa Mzani wa Bwanga, wilayani Chato, Daudi Kadikilo (47), kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela na kulipa faini ya Sh. milioni 3.5.

Hukumu hiyo imetolewa baada ya kukutwa na hatia katika makosa ya kushawishi Sh. milioni moja na kupokea hongo ya Sh. 300,000 kinyume cha 15(1)(a) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Hukumu hiyo imetolewa jana na Hakimu wa Mahakama hiyo, Erick Kagimbo, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa manne pasipo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Kagimbo alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo, ili iwe fundisho kwake na kwa wafanyakazi wengine wenye tabia kama yake.

Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri, alidai mahakamani kuwa alipeleka mashahidi wanane na vielelezo saba ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa alitenda makasa hayo.

Alidai kuwa mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa Wakala wa Barabara (Tanroad) Mkoa wa Geita, alikamata roli lenye namba za usajiri T 602 DLE na baada ya kukamata gari hilo, alishawishi hongo ya Sh. milioni moja lakini walikubaliana Sh. 300,000 na kati fedha hizo, alipokea Sh. 100,000 kutoka kwa Fabian Shigadu.

Baada ya kupokea fedha hizo, Shigadu alikwenda ofisi za TAKUKURU Chato na kutoa taarifa ndipo ofisa wa TAKUKURU alimwambia mlalamikaji amtumie Sh. 100,000 kwenye M-pesa ya mshtakiwa.

Alidai kuwa baada ya kumtumia, alimwambia fedha nyingine atachukuwa jioni na ilipofika majira ya jioni, mlalamikaji alichukuwa fedha za mtego na kufanikisha kukamatwa kwa mshtakiwa huyo.

Aidha, ilidaiwa kuwa baada ya kufanya upekuzi kwenye gari lake aina ya Suzuki lenye namba za usajili T 176 DMP walizipata fedha za mtego Sh. 100,000 mali ya TAKUKURU Wilaya ya Chato.

"Nimeangalia ushahidi wa pande zote nimegundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha makosa yote manne pasipo kuacha shaka yoyote na mshtakiwa umetiwa hatiani kwa makosa yote manne. Pia mahakama hii inakutaka ujitetee, ili iweze kukupunguzia adhabu," alisema Hakimu Kagombo.

Mshtakiwa huyo aliangua kilio na kuomba mahakama inipunguzie adhabu kwa kuwa ana familia inayomtegemea pia ana mama yake ni mjane anaomba mahakama impe adhabu ndogo sana.

Upande wa mashtaka uliomba mahakama itoe adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo, ili kukomesha vitendo vya rushwa vilivyokithiri na kuathiri barabara zinazojengwa kwa kodi za Watanzania wanyonge.

Hakimu Kagimbo alitupilia mbali utetezi wa mshtakiwa na kusema kosa la kwanza mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka mitatu jela au faini ya Sh. 900,000 na kosa la pili mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka mitatu jela au faini ya Sh. 800,000.

Kwa kosa la tatu, alisema mshtakiwa atatumikia miaka mitatu jela pamoja na kulipa Sh. milioni moja, huku kosa la nne akipewa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu jela au faini ya Sh. 800,000.

Hakimu Kagimbo alidai hapo mahakamani kuwa gari ya mshtakiwa aina Suzuki yenye namba za usajili namba T 176 DMP pamoja na simu aina ya Tecno G. ZNI vyote vimetaifishwa na kuwa mali ya serikali kwa sababu vimehusika kwenye utendaji wa makosa hayo ya rushwa.

## Makinda atoa siri kudumu udiwani

**Na Yasmine Protace**

ANNA Makinda, Spika wa Bunge la 10, amesema madiwani ambao wanataka kurudi katika nafasi zao, wanatakiwa kuwatumikia wananchi kwa kuwa ndiyo wenye mamlaka ya nafasi hizo.

Amesema kuwa bila kuwaletea maendeleo wananchi, wajue awamu nyingine hawatachaguliwa kutetea nafasi zao hizo za kisiasa.

Makinda aliyasema hayo wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo madiwani wanawake yaliyoandaliwa na TGNP Mtandao.

"Ili turudi katika nafasi zetu za udiwani kwa awamu nyingine, kinachotakiwa ni kuwatumikia wananchi ambao ndiyo wametuchagua," alisema.

Makinda aliongeza kuwa mafunzo waliyoyapata, wanapaswa kuyatumia vizuri ili kuwaletea maendeleo wananchi wao.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Lihundi, alisema wana programu maalumu ya wanawake na uongozi inayolenga kuongeza ushiriki kwa wanawake katika ngazi za uamuzi wa kisiasa kuanzia mwaka 2021 hadi 2025. Aliongeza kuwa programu hiyo inaendelea kuwajengea uwezo madiwani na kuendelea kufanya nao kazi kwa pamoja.

"Katika programu hii, tunaangalia madiwani wanahitaji nini kwa ajili ya kuwajengea uwezo ambao utawasaidia kuwaletea maendeleo katika maeneo yao," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa katika programu hiyo ya miaka mitano, kutakuwa na programu ambayo inazungumzia mambo ya malezi na ukungwi.

Kwa mujibu wa Lihundi, madiwani 70 kutoka mikoa tisa, wamepatiwa mafunzo ya kutumia takwimu ambazo zitawasaidia kufanya kazi zao kwa weledi na wanafundishwa kutafuta rasilimali ili watatue matatizo ya wanawake katika maeneo yao ya kazi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na viongozi wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) kwenye ukumbi wa ofisi ndogo ya Waziri Mkuu, Magogoni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## Mlinzi mbaroni tuhuma kuua mke

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza, linawashikilia watu wanane kwa tuhuma za kufanya makosa mbalimbali yakiwamo mauaji, kupatikana na bangi na uporaji.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Mwanza jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Jumanne Muliro, alisema watuhumiwa hao kwa sasa wanashikiliwa na jeshi hilo kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Alisema kuwa Benson Oluochi (54), mkazi wa Mtaa wa Capripoint jijini, ambaye ni mlinzi wa kampuni binafsi, anashikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma za kumuua mke wake, Elizabert Benson.

Kamanda Muliro alidai kuwa chanzo cha ugomvi huo ni madai ya kukosa uaminifu ndani ya ndoa.

Alisema mtuhumiwa anadaiwa kumshambulia kwa fimbo sehemu mbalimbali za mwili mke wake mpaka akapoteza maisha.

"Elizabert (45), mkazi wa Capripont, alifanyiwa ukatili huo Desemba 20 mwaka huu majira ya saa 11 jioni na alifariki dunia muda mfupi baada ya kufikishwa Hospitali ya Sekou Toure kwa ajili ya matibabu," alisema.

Katika tukio lingine, jeshi hilo linamshikilia Sitta Gabunga (66), mkazi wa Igombe jijini kwa kosa la kupatikana na magunia matano ya bangi na misokoto 30.

Katika tukio la tatu, watu sita wanashikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma za uporaji wa vitu mbalimbali ikiwamo pikipiki yenye namba za usajili MC 971 CDU, viambaza (screen) vitatu, solar aina ya Sundar na redio.


TAARIFA KWA UMMA



JINA: SAID ILONGA

MKAZI WA: DAR ES SALAAM

Tunapenda kuutarifu umma kuwa mtajwa hapo juu ndugu Said Ilonga alikua mtumishi katika kampuni ya Selcom kwa sasa sio mfanyakazi wa kampuni hii tena, na kuwa hatutahusika na kazi au taarifa zozote zitakazofanywa na mtu huyu, na wala yeye hatohusika na kazi, mazungumzo ya kifedha au taarifa zozote zitakazohusiana na Selcom.

Kama kutakua na taarifa zozote tofauti tafadhali wasiliana na info@selcom.co.tz

# Katibu hospitali jela miaka mitano ununuzi wa dawa, vifaa tiba hewa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, imewahukumu maofisa wawili wa afya na mzabuni kutumikia kifungo cha miaka mitano jela na kurudisha Sh. milioni 32.7 kwa ununuzi hewa wa dawa na vifaa tiba.

Washtakiwa hao walishtakiwa kwa makosa manne ya kutumia vibaya madaraka, kutumia nyaraka kumdanganya mwajiri, kujipatia manufaa yasiyostahili na kuisababishia serikali hasara ya Sh. 32,700,000 kinyume cha sheria.

Washtakiwa hao ni Nathalia Berthold (36) ambaye ni Katibu wa Afya wa Hospitali Wilaya ya Geita, George Matundali (46) Mhasibu wa Idara ya Afya, na David Magira (53) mmiliki wa Magira Pharmacy iliyoko jijini Mwanza.

Washtakiwa hao walifika hapo mahakamani majira ya saa 3:00 asubuhi na kupandishwa kizimbani saa 6:00 mchana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Obadia Bwegoge, kisha kusomewa hukumu kwa saa mbili na kutolewa uamuzi.

Katika hukumu hiyo, Hakimu Bwegoge alisema anatoa adhabu hiyo baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa yote manne pasipo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Bwegoge alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao, ili iwe fundisho kwao na watumishi wengine wenye tabia kama yao.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri, alipeleka mashahidi sita na vielelezo 5 ambavyo vilithibitisha kuwa washtakiwa wote kwa pamoja walitenda makosa hayo.

Alidai kuwa Januari 24, 2014 washtakiwa wote watatu walishirikiana kuandaa hati za malipo kudai kwamba dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. 32,700,000 vimenunuliwa na kupokewa katika hospitali hiyo wakati si kweli.

Kutokana na madai hayo Murusuri aliomba mahakama iwape adhabu washtakiwa hao kwa mujibu wa sheria.

Alidai kuwa mshtakiwa wa kwanza, Berthold (36) na wa pili Matundali (46), walitumia madaraka yao vibaya na kutumia nyaraka kumdanganya mwajiri kwa kuandaa hati za malipo zenye thamani ya Sh. 32,700,000 kwa ajili ya mshtakiwa wa tatu, Magira (53) kwa kudai kwamba dawa na vifaa tiba hivyo vimepokewa katika Hospitali ya Wilaya ya Geita.

Murusuri alidai kuwa washtakiwa walitenda kosa hilo kinyume na kifungu cha 31 na 22 cha Sheria Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Aliendelea kudai mahakamani hapo kuwa tarehe hiyo hiyo, Magira alijipatia malipo yasiyostahili kinyume cha kifungu cha 23 (1)(a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Mwendesha mashtaka huyo alidai kwamba washtakiwa wote watatu waliisababishia serikali hasara ya Sh. 32,700,000 kinyume na aya ya 10 (1) ya jendwali la kwanza kifungu cha 57 (1) na 60 (2) ya Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.



Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa daraja linalounganisha Ubungo na Mawasiliano, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwambe awapa mwanya sekta binafsi

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Godfrey Mwambe, amewataka wadau wa sekta binafsi kuchangamkia fursa katika mazao ya kilimo.

Alisema zipo fursa nyingi katika sekta hiyo ambazo wadau wakizichangamkia ipasavyo upo uwezekano wa wao kuwa mabilionea.

Alitoa kauli hiyo wakati akizindua Bodi mpya ya Wakurugenzi wa TPSF katika mkutano wa 20 wa taasisi hiyo uliofanyika jana jijini Dar es Salaam na kumchagua mwenyekiti atakayeongoza kwa miaka miwili.

"Mabilionea wazalendo watatengenezwa kupitia sekta binafsi kwa kuzifanyia kazi fursa zilizopo hususani kutafuta masoko ya nje ya mazao ya kimkakati ili kutengeneza wigo wa kukuza na kuendeleza biashara nchini," alisema Mwambe.

"Mfano zao la korosho, kuna zaidi ya tani laki mbili zimekosa mnunuzi wa nje kwa sababu ya soko, kwa hiyo sekta binafsi ina uwezo wa kununua zao hilo kutoka kwa wakulima wadogo na kutafuta soko nje ya nchi na litachochea ukuaji wa uchumi kutoka ngazi ya mkulima mpaka kwa wafanyabiashara."

Mwambe alisema tatizo la ukosefu wa soko la uhakika, lipo pia katika mazao yote ya kimkakati ikiwamo pamba, kahawa, tumbaku, chai na korosho na kuna kila sababu kwa sekta binafsi kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuhakikisha malengo ya serikali ya kuimarisha uchumi wa kati yanatekelezeka.

"Imani yangu kwa bodi hii mpya iliyochaguliwa leo itakwenda kutekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa masoko ya mazao haya ya mkakati ili yapate soko la uhakika."

Kwa upande wake Mwenyekti mpya wa Bodi ya TPSF, Angelina Ngalula, alisema taasisi hiyo haitakuwa tayari kuwakumbatia wafanyabiashara wanaovunja maadili ya kibiashara nchini.

"Lengo letu ni kulinda taswira ya TPSF mbele ya umma, serikali na wanachama wenyewe na hatua zitakazokuwa zinachukuliwa kwa wanaokiuka maadili ya kibiashara yatakuwa ni kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo," alisema Ngalula.

"Pia TPSF ya sasa haitowaacha nyuma vijana wanaohangaika katika biashara ndogo kwa kuhakikisha wanatambuliwa ndani ya taasisi na kuwawezesha kwa kuwaunganisha na fursa mbalimbali ikiwamo mikopo ili kukuza mitaji yao."

## Bugando watibu watoto waliokosa sehemu haja kubwa

**Na Richard Makore,** MWANZA

MADAKTARI bingwa kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando pamoja na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), wamefanikiwa kufanya upasuaji kwa watoto 42 waliozaliwa bila kuwa na sehemu za haja kubwa.

Katika upasuaji huo, madaktari bingwa walifanikiwa kupasua watoto hao na kuwawekea sehemu za haja kubwa ambazo sasa watazitumia kutolea haja hiyo.

Upasuaji huo wa kibingwa ulifanyika jana katika Hospitali ya Bugando jijini Mwanza chini ya madaktari bingwa wa Bugando na Muhimbili. Akizungumza jana jijini, Dk. Samuel Byabato, ambaye ni daktari bingwa kutoka Hospitali ya Bugando alisema, upasuaji huo ulianza Desemba 17 mwaka huu na ulifanywa na jopo na madaktari bingwa tisa.

Alisema katika miaka mitano iliyopita, hospitali hiyo imeboresha huduma za tiba na kwamba kwa sasa wana jumla ya vyumba vya upasuaji 13. Dk. Byabato alisema kutokana na kuboreshwa kwa huduma hizo, kwa sasa idadi ya wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji imefikia 1,200 kwa mwezi kutoka 750 siku za nyuma.

Dk. Petronila Ngiloyi ambaye ni daktari bingwa wa watoto kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, alisema lengo la huduma hiyo ni kupunguza gharama za wagonjwa wanaopewa rufani kwenda Dar es Salaam katika Hospitali ya Taifa ya Taifa Muhimbili kwa ajili ya matibabu ya kibingwa.

Mmoja wa wazazi ambao watoto wao walipatiwa huduma hiyo, Kassa John, mkazi wa mjini Musoma mkoani Mara, alishukuru serikali kwa kuwapatia matibabu hayo ya kibingwa.

## Majaliwa achagiza mchango wa TPSF

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ndicho chombo muhimu na chenye mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ya kiuchumi Tanzania.

Aliyasema hayo jana, alipokutana na bodi mpya ya taasisi hiyo katika ukumbi wa Ofisi Ndogo ya Waziri Mkuu, Magogoni jijini Dar es Salaam.

Kikao hicho ni utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Rais John Magufuli alipozindua Bunge la 12, jijini Dodoma, kuhusu ushirikiano kati ya serikali na TPSF.

Viongozi wa taasisi hiyo waliishukuru serikali kwa ushirikiano inaowapatia ambao unawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa urahisi na ufanisi mkubwa.

## Naibu waziri ataka watumishi wauziwe nyumba bei nafuu

**Na James Mwanamyoto**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ameitaka Kampuni ya Watumishi Housing kuacha kuendelea kutumia makandarasi katika miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za kuwauzia na kuwapangisha watumishi wa umma, badala yake itumie utaratibu wa 'force account' ili kuokoa gharama na kujenga nyumba ambazo watumishi watamudu kupanga na kuzinunua.

Deogratius Ndejembi alitoa agizo hilo jana wakati wa ziara yake ya kikazi yenye lengo la kufahamiana na watumishi wa taasisi hiyo na kukagua miradi inayotekelezwa na taasisi zilizo chini ya ofisi yake.

Alisema madhumuni ya kuanzishwa kwa Watumishi Housing Company ni kujenga nyumba za gharama nafuu zinazoweza kununuliwa na watumishi wa kada zote, hivyo hakuna sababu ya kutumia makandarasi ambao gharama zao za ujenzi ni kubwa na kusababisha gharama kubwa za upangishaji na uuzaji wa nyumba hizo.

"Watumishi wa umma wanajitoa sana katika kulitumikia taifa hili, sasa ni wakati wa serikali kutambua mchango wao kwa kuwawezesha ikiwa ni pamoja na kuwapatia nyumba za gharama nafuu," Ndejembi alisema.

Aliongeza kuwa, kuna majengo mbalimbali ya serikali yaliyojengwa kwa ubora kwa kutumia 'force account', akitolea mfano baadhi ya majengo hayo ambayo yako katika Mji wa Serikali-Mtumba kuwa ni ya Ofisi za Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Company, Dk. Fred Msemwa, alisema wamepokea maelekezo ya naibu waziri huyo kutumia 'force account' na wameshajiandaa kwa ajili ya hilo.

# Silinde awapa kibarua maofisa elimu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, David Silinde, amewaagiza maofisa elimu na wakurugenzi wa halmashauri kushughulikia kero ya uhaba wa madarasa, ili wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wote waanze masomo kwa wakati.

Aidha, amewataka kuweka kipaumbele katika kukabiliana na kero na si kuwa kama dharura kwao. Silinde pia amewaagiza watendaji hao kusimamia miundombinu ya elimu pamoja na fedha zinazotolewa na serikali katika ujenzi ili zitumike kikamilifu.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga mkutano wa saba wa maofisa elimu wa mikoa na wilaya uliofanyika jijini hapa.

Watendaji, alisema hawapaswi kumwangusha Rais John Magufuli kutokana na jitihada zinazofanywa na serikali za kujenga miundombinu ya elimu na kuboresha ili kuhakikisha sekta hiyo inaimarika.

"Ninaamini kikao hiki kina manufaa kwenu na mmejadili mambo ya msingi katika elimu na mkayafanyie kazi ili kuinua kiwango cha elimu kama kaulimbiu yenu inavyosema," alisema Silinde.

Pia alisema wakati serikali ikiendelea na jitihada za kutatua changamoto hiyo, wakiwa wasimamizi katika maeneo yao, wahakikishe suala hilo linamalizika kupitia mfumo wa 'force account'.

"Kwa muda wote mliokaa hapa natumai mtakuwa mmeelewa umuhimu wenu na serikali kwa ujumla, katumieni fedha iliotolewa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ikalete thamani," alisema Silinde.

Alisema wanapaswa kwenda kumalizia miundombinu ya elimu, ujenzi wa vyoo, madarasa na kuzingatia watu wenye ulemavu. Kuhusu walimu wanaopangiwa vituo vya kazi, alisema wanapaswa kupokewa na kuonyeshwa maeneo husika ya kufanyia kazi.

"Walimu wanapaswa kupokewa vizuri na kupewa ushirikiano katika masuala ya kazi hivyo ni vema wakapewa ushirikiano," alisema Silinde.

Sambamba na hayo, aliwataka kuimarisha misingi ya kazi, uwajibikaji pamoja na kuonyesha uzalendo wa kitaifa kwa kuimarisha ubora wa walimu wa shule za msingi.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mhandisi Joseph Nyamuhanga, aliwasisitiza maofisa hao kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa kabla ya Februali 28, mwakani ili kumaliza kero hiyo.

Nyamuhanga alisema serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya kuboresha miundombinu, hivyo shule zote kongwe za sekondari zimekarabatiwa.


The Guardian www.ippmedia.com
Nipashe MWANGA WA JAMII www.ippmedia.com




For our
Advertisement Customers

| Just pay for your Print advertisement | Get Free | | | |
|---|---|---|---|---|
| Size of Advertisement | Free E-Paper for One Month | | Free Social Media Post | |
| | The Guardian | Nipashe | Guardian or Nipashe | Guardian or Nipashe |
| Full Page | 10 E-Papers | 10 E- papers | 5 Posts | 5 Posts |
| 3/4 Page | 7 E- Papers | 7 E - Papers | 2 Posts | 2 Posts |
| 1/2 Page | 5 E- Papers | 5 E- papers | 2 Posts | 2 Posts |
| 3/8 Page | 3 E- Papers | 3 E- Papers | 1 Post | 1 Post |
| 1/4 Page | 2 E- Papers | 2 E- Papers | 1 Post | 1 Post |



For More Information Please Contact us:
0782 253 676 advertise@guardian.co.tz

1. This offer is Valid till 31st Dec 2020
2. Terms and conditions apply

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Chonde chonde sikukuu zipite zikituacha salama

**SIKUKUU** za Noeli na Mwaka Mpya zimewadia na pengine karibu kila mmoja anaendelea na kujiandaa ili kujipa furaha na familia yake.

Kwa wanaojiandaa kwa mkesha wa Noeli kesho jioni tunawatakia kila la heri pamoja na ibada zilizojaa upendo, amani na furaha.Aidha, tunawatakia wote maandalizi mema na kuwakumbusha kuwa yale mambo ya zamani kuwa sikukuu ndizo nyakati za kujifurahisha kupindukia, sasa fikra hizo tuzibadilishe.

Tunasema hayo tukikumbuka enzi zile ambazo pengine haukuwako mwongozo hali iliyosababisha wengi wakadhani kuwa kufanya mambo kupitiliza ndiko kujifurahisha na kula sikukuu kikamilifu. Wapo waliolewa kupindukia, kuendesha magari kwa fujo na mambo mengine yasiyo na maadili.

Lakini miaka ya sasa kila mmoja anafahamu umuhimu wa kujilinda binafsi, familia na jamii yake. Tunasisitiza umuhimu wa kuwalinda watoto na kuwaepusha na majanga ambayo pengine hayakuwa na sababu ya kutokea.

Walezi na wazazi wahakikishe kuwa hawawaachi watoto kuzurura kupindukia, kuzagaa na kudhalilishwa kwani sikukuu za mwisho wa mwaka ndicho kipindi wengi wanapojisahau na kuacha watoto kuingia kwenye matatizo au majanga.

Tukumbuke huu si wakati wa kuwaacha watoto kucheza mbali na nyumbani, kuwasafirisha kwenda maeneo ambayo hatuwaoni hasa vijijini au kwa jamaa wengine mijini, kwa vile kunaweza kusababisha athari. Tufahamu wanaweza kudhalilishwa, kuibwa, kunyweshwa pombe na hata kuuawa, hivyo ni wito wetu kila mmoja kuwalinda sana watoto na wale wasiojiweza wakiwamo wagonjwa wa akili, wenye ulemavu na wazee.

Tunafahamu katika kusherehekea, ndiyo msimu wa kutembelea maeneo ya ufukweni na sehemu za burudani. Si jambo baya, lakini tunawakumbusha umakini.

Wahudumu wa sehemu za baharini, hotelini, ukumbini, walezi na wazazi wawe makini watoto wanapokuwa maeneo hasa kwenye kuogelea. Tukumbuke kuwalinda na kuwachunga watoto kuepusha majanga hasa ya kuzama baharini.

Tukumbushane kuwa tunahitaji pia kujihakikishia usalama wa nyumbani tunapoishi na mali zetu. Tusitembelee maeneo yenye wahalifu, wezi wa simu, wavuta bangi na wakabaji.

Ndiyo maana tunawashauri kila mmoja kutojisahau, tukizingatia kuwa hiki ndicho kipindi mifugo inapoibwa kuuzwa kitoweo cha sikukuu. Ni vyema tukachukua tahadhari na kuwa makini badala ya kuwaachia watumishi au wafanyakazi wetu kuangalia kila kitu.

Hakika kula na kunywa hakuepukiki, lakini tuwe makini na tunachokunywa au kula kwa vile upo uwezekano wa kutumia vinywaji na vyakula visivyo salama, vinavyoweza kutudhuru.

Ajali barabarani pia ni chanzo cha vifo, ulemavu na uharibifu wa mali zetu. Tusijisahau, kunywa na kuendesha gari, pikipiki au bajaji kwa fujo kunakochangia matatizo hayo.

Tunapokwenda kwenye sikukuu tukumbuke kuna maradhi ukiwamo Ukimwi kwa kuwa maambukizi mapya yapo na yanaendelea kurekodiwa, tujiepushe. Mathalani, watu 72,000 wanaelezwa kuwa wanaambukizwa kila siku ikimaanisha kuwa kuna kujamiana kusikojali usalama na afya za wahusika.

Tukumbuke kuwa mambo ni mabaya zaidi kwa wanawake wakiwamo wasichana na mabinti ambao ni waathirika zaidi.

Hawa wanaelezwa kuwa ni wale vijana wenye umri kati ya miaka 14 hadi 35, wanaotajwa katika maambukizi mapya. Tuwalinde watoto ambao pamoja na athari hizo wanakwamishwa kimasomo.

Ni wito wetu kwa kila mmoja tuwe na kiasi, tulinde maisha yetu na ya wengine ili tumalize kwa usalama sikukuu hizi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mazungumzo yaanze mvutano 'usichache'

**MVUTANO** kati ya Bunge, Tume ya Uchaguzi (NEC) na CHADEMA unaoendelea kufukuta baada ya wabunge 12 kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum na kufutwa uanachama, ni jambo linalohitaji hitimisho sasa.

Wabunge hao akiwamo Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA, Halima Mdee, na wenzake Stella Fiao, Grace Tendega, Esther, Matiko, Cecilia Pareso, Ester Bulaya na Agnesta Lambart.

Wapo pia Conchesta Rwamlaza, Nusrati Hanje, Jessica Kishoa, Hawa Mwaifunga, Kunti Majala, Tunza Malapo, Asia Mohammed, Felister Njau, Naghenjwa Kaboyoka, Sophia Mwakagenda, Anatropia Theonest na Salome Makamba.

Tukio la kuapishwa kwao jijini Dodoma lilikuwa la kushtukiza, kwa kuwa baadhi ya watu hawakutarajia lingetokea, kutokana na kwamba uongozi wa juu wa chama hicho ulishaweka wazi kuwa hakutakuwa na ushiriki wowote wa wabunge wa viti maalum.

Lakini si mara ya kwanza upinzani nchini kutotambua matokeo ya uchaguzi, na kuruhusu wabunge wake kushiriki vikao vya bunge, ila safari hii kumekuwapo na mvutano ambao ni vyema upatiwe ufumbuzi.

Wabunge hao wameondolewa katika chama, lakini wanadai kwamba, bado ni wanachama halali wa CHADEMA.

Aidha, wanasema wako mbioni kukata rufani katika ngazi mbalimbali za chama kama inavyoelekezwa na katiba yao.

Huo ni mvutano kati yao na uongozi wa chama, na pia NEC na Bunge wanaopigilia msumari wa kuwatambua kama wabunge halali, kwa maelezo kwamba, taratibu za kupatikana kwao zilifuatwa.

Mkurugenzi wa NEC, Dk. Charles Mahera, ananukuliwa na vyombo vya habari, akisema chama hicho kiliwasilisha majina ya wabunge wa viti maalum.

Anakariri vifungu alisema: "Kwa mujibu wa ibara ya 78 ya katiba ya nchi, kipengele cha 3, majina ya watu yaliopendekezwa kwa mujibu wa ibara ndogo ya kwanza, yatatangazwa baada ya NEC kuridhika kwamba masharti ya katiba na sheria yamezingatiwa."

Lakini CHADEMA inashikilia msimamo wake kwamba, haijateua majina ya wabunge wa viti hivyo kimemwandikia barua Spika wa Bunge ya kuwakana wabunge hao walioapishwa.

Hata hivyo, Bunge linawataka viongozi wa chama hicho kwenda NEC au mahakamani na kusisitiza kuwa wote 19 ni halali, kama hawajaridhika kuhusu mvutano huo ambao umeleta mkanganyiko.

Wachambuzi wa masuala ya siasa wanasema, majina ya wabunge wa viti maalumu wa chama hupelekwa kwa Spika na katibu mkuu wa chama husika.

Hata hivyo, katika tukio hilo, inasemekana, John Mnyika, ambaye ni Katibu Mkuu wa CHADEMA, hakuandika barua kama utaratibu ulivyo na hadi sasa haijawekwa wazi ni nani aliyeiandika.

Kutokana na utata na mvutano uliopo sasa Muungwana anaona ipo haja kwa pande zote akiwamo na hata Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kukutana na kuweka sawa.

Hatua hiyo inaweza kusaidia kupatikana kwa muafaka wa mvutano huo, kwa kuwa jambo litawekwa wazi na ukweli utajulikana badala ya kuendelea na mgogoro unaelekea kuchacha kwani hauna afya kidemokrasia.

Ikumbukwe kuwa ibara 21, 39, 47 na 67 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa haki ya mtu kuwawakilisha wananchi katika ngazi za maamuzi kwa sharti la kupitia au kudhaminiwa na chama cha siasa.

Ibara ya 71(1)(e), inasema, mbunge atakoma kuwa mbunge na ataacha kiti chake katika bunge endapo ataacha kuwa mwanachama wa chama alichokuwamo wakati alipochaguliwa au alipoteuliwa kuwa mbunge.

Wadau wakikutana na kufafanua zaidi vifungu hivyo, wanaweza kupata muafaka kwenye mvutano, kwa kuwa kila upande utasikilizwa na na kitendawili kitatatuliwa.

Kukutana kwao kutasaidia kutafsiri vifungu vya katiba ya nchi, sheria, kanuni na tarabu, hasa kwa kuzingatia kwamba suala la udhamini wa chama cha siasa katika ngazi za maamuzi ni takwa la msingi la kikatiba.

Kwa hali hiyo, njia bora ya kumaliza migogoro au tofauti, ni meza ya mzungumzo, kwa kuwa inawezekana wote lengo lao ni moja ila kuna sehemu ndogo wanayotofautiana.

HABARI KITAIFA

## Bilioni 15.9/- kutumika miradi maji Mwanza

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Mwanza, imepanga kutelekeza miradi 45 inayotarajia kugharimu Sh. bilioni 15.9.

Kwa mwaka wa fedha wa 2020/21 katika Mkoa wa Mwanza, RUWASA imepanga kutelekeza miradi hiyo kulingana na fedha zilizoidhinishwa.

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa RUWASA Mkoa wa Mwanza, Emmaculata Raphael, wakati akiwasilisha taarifa katika kikao cha kwanza cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Mwanza kwa mwaka wa fedha wa 2020/21 kilichofanyika mkoani hapa.

Alisema miradi mitano inatekelezwa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando.

Meneja Msaidizi Miundombinu wa MWAUWASA, Stanley William, akiwasilisha taarifa ya hali ya huduma ya maji, alisema kaya 4,705 za jijini Mwanza zimeunganishwa katika mfumo wa uondoaji wa majitaka.

William alisema kutokana na jiografia ya Jiji la Mwanza kuwa ya miinuko majitaka husafirishwa kwa kusukumwa na pampu zilizofungwa katika vituo vitatu.

## Watakiwa kuchangamkia mgambo

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

WANAWAKE wenye sifa za kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Akiba katika Mkoa wa Singida, wameshauriwa kutoyakimbia na badala yake wajitokeze kwa wingi kushiriki kikamilifu.

Wito huo ulitolewa juzi na mmoja wa wahitimu wa mafunzo jeshi hilo, Manispaa ya Singida, Asha Saidi, wakati wa kuhitimu mafunzo hayo katika viwanja vya michezo vya Mandewa.

Asha alisisitiza kwamba idadi kubwa ya kinadada wamekuwa wakiogopa kujiunga katika mafunzo hayo na kuhamia kabisa kwenye vijiji ambavyo hayatolewi mafunzo hayo.

Mhitimu huyo alitumia fursa hiyo kutoa wito kwa kinadada wengine kuondokana na dhana iliyozoeleka ya kuzikimbia nyumba na familia zao na kwamba fursa kama hizo zinapotolewa wasisite ili kupata faida binafsi, familia na hata taifa kwa ujumla.

Mariam Iddi aliweka bayana kuwa kutokana na mafunzo hayo, anaamini amekuwa tofauti sana na wengine ambao hawajawahi kujiunga kwa kuwa wanafundishwa mbinu nyingi za kukabiliana na maadui.

# Gekul aonya uvuvi haramu

**Na Mbaraka Kambona,** BABATI

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, amewaonya watu wanaojihusisha na uvuvi usiozingatia sheria na taratibu na kuwataka kuacha mara moja, kwa kuwa serikali haitakuwa na huruma kwa watakaokamatwa.

Gekul alitoa onyo hilo alipokuwa akiongea na wavuvi wa Mkoa wa Manyara, alipofanya ziara mkoani humo juzi.

Kwa mujibu wa Waziri Gekul, katika operesheni ya kupambana na uvuvi haramu iliyopita, ilitumika karibu Sh. bilioni 1.2 jambo ambalo alisema halivumiliki na kuwataka wavuvi kutoa ushirikiano kwa serikali ili kukomesha vitendo hivyo.

"Hatutavumilia jambo hili liendelee, sisi kama wizara tumesema ni lazima tupate mwarobaini wa uvuvi haramu, lakini na nyinyi wavuvi muwe tayari kutoa ushirikiano kwa serikali ili uvuvi haramu ukomeshwe mara moja," alisema Gekul.

Alisema, uvuvi haramu ukikomeshwa itasaidia kuokoa mazalia ya samaki na kuongeza idadi yao katika maziwa na maeneo mengine.

"Kwa kuwa mmeonyesha nia ya kutoa ushirikiano katika hili, shirikianeni na viongozi wenu kuanzia leo (juzi) hizo nyavu haramu zikatupwe, tusisikie tena kuhusu nyavu haramu iwe mwanzo na mwisho," aliongeza Gekul.

Vile vile, alisema kipaumbele cha serikali kwa sasa ni kuimarisha ufugaji wa viumbe maji kwa kutumia vizimba na mabwawa jambo ambalo alisema likisimamiwa vizuri litaongeza ajira kwa wananchi, kupunguza umaskini na kuchochea uchumi wa taifa.

"Niwaombe wakurugenzi na viongozi wengine wa halmashauri waangalie uwezekano kwenye zile asilimia kumi zinazotolewa na serikali kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu badala ya kuwapa mkononi wafanye utafiti, ili kujua ujenzi wa mabwawa unagharimu kiasi gani ili wawajengee mabwawa ya kufugia samaki na tukiweza kufanya hivyo tutakuwa tumepunguza tatizo la ajira," alisisitiza Gekul.

Katika hatua nyingine, aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri na maofisa uvuvi kuwafikia wavuvi wote na kuhakikisha wanalipia leseni za uvuvi, ili kuzuia upotevu wa mapato na kukuza pato la serikali.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema kuwa maelekezo yote yaliyotolewa na Naibu Waziri wameyapokea na watayafanyia kazi kama ilivyoelekezwa ili sekta ya uvuvi mkoani humo iweze kupiga hatua inayotarajiwa.

Mwenyekiti wa Wavuvi, Halmashauri ya Babati, Iddi Hassani, alisema kuwa watafanyia kazi maelekezo na watahakikisha wanashirikiana na serikali ili wavuvi wote wawe na leseni za uvuvi na wataendelea kupambana na uvuvi haramu ili kunusuru viumbe maji na kuendelea kufanya uvuvi endelevu.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (kulia), akipokea samaki sato kutoka kwa Mkurugenzi, Idara ya Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Magese Bulayi, alipotembelea kampuni ya XIN SI LU kutoka China, iliyowekeza katika ufugaji wa samaki kwenye mabwawa mkoani Manyara. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# Waziri amweka kitomoto mhandisi maji

**Na Steven William,** PANGANI

MHANDISI Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Pangani, Yahaya Rajabu, juzi, alijikuta katika wakati mgumu baada ya kuwekwa kitimoto na Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, kutokana na kusimama kwa miradi ya maji kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Naibu Waziri huyo alifika katika Wilaya ya Pangani mkoani Tanga, juzi, kukagua na kuweka mawe ya msingi ujenzi wa miradi miwili ya maji inayosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa

Mazingira Tanga (Tanga UWASA) katika kijiji cha Msalaza na ule wa kijiji cha Mbulizaga.

Baada ya kuwasili, alisomewa taarifa na mhandisi huyo na kueleza kuwa ujenzi wa miradi hiyo umesimama kutokana na fedha kuchelewa kufika.

Kutokana na taarifa hiyo, Naibu Waziri alisema haiwezekani ujenzi wa miradi hiyo kusimama na ni kosa kubwa kwa sababu ya fedha na kwamba serikali imeleta fedha.

Mahundi alisema mhandisi huyo anafanya kazi kwa mazoea na sasa hawezi kwenda na kasi ya serikali, hivyo ajitafakari.

Alisema wananchi wa vijiji vya Bushiri na Mbulizaga wanataka majisafi na salama sasa anashangaa kuambiwa mradi huo umesimama kwa muda wa mwezi sasa kwa kisingizio cha fedha wakati fedha kwa ajili ya miradi hiyo zipo.

Kutokana na hali hiyo, aliagiza miradi hiyo kuanza tena kuanzia jana na hataki kuona mabomba yakiwa yamerundikwa na mradi umesimama huku. Mahundi alitoa miezi sita miradi hiyo iwe imekamilika na wananchi wanapata maji, huku mabomba yakifika mpaka ndani ya nyumba.

Diwani wa Mkalamo, Rajabu Mipango, alisema mradi wa maji katika kijiji cha Mbulizaga umesimama ujenzi wake kwa mwezi sasa na vibarua ambao wanafanya kazi wanadai fedha nyingi, hivyo wanakata tamaa ya kufanya kazi.

Kutokana na taarifa hiyo, Naibu Waziri Mahundi aliagiza vibarua hao walipwe mara moja fedha zao.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Tanga, Upendo Lugongo, alisema fedha za miradi hiyo ya maji zipo na kwamba zitapelekwa kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa haraka na kuahidi kwamba hadi kufikia Machi, mwakani, itakuwa imekamilika na wananchi wanapata maji.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, Akida Bahorera, alisema Mbunge wa Pangani, Jumaa Aweso, anapigania sana Jimbo la Pangani kupata miradi mbalimbali ikiwamo ya maji, lakini watendaji wanakwamisha ujenzi wa miradi hiyo.

# Wavuvi haramu watangaziwa kiama

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imetangaza kiama kwa wavuvi haramu wote, ikibainisha kuwa sasa inakuja na msako endelevu na kuondokana na ule uliokuwa ukifanywa mara moja moja.

Imetangaza kufanya msako huo kwa kuwatafuta mahali popote walipo wale wote wanaoendesha uvuvi huo na kuwachukuliwa hatua kali za kisheria.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alitangaza hayo jana alipokuwa katika mkutano wa hadhara na wakazi wa Kijiji cha Mchinga Namba Mbili, kilichoko wilayani Mchinga mkoani Lindi wakati wa ziara yake mkoani huko.

Alisema operesheni hiyo itakuwa shirikishi katika mikoa na wilaya zote ambazo shughuli hizo za uvuvi haramu hufanyika.

"Tunataka operesheni hii iwe endelevu na siyo ya zimamoto, tunataka kumaliza kabisa tatizo la uvuvi haramu na tunaamini hili litabaki historia.

"Niwatahadharishe wale wote wanaojihusisha na uvuvi huo haramu na wanaofikiria kujiingiza huko, kwa sababu hatutawaacha salama, tutawatafuta popote watakapokuwa na watapata adhabu kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za nchi hii," alionya.

Ndaki alisema kuwa pamoja na jitihada ambazo zimekuwa zikifanywa na serikali katika kupambana na vitendo hivyo vya uvuvi haramu, bado vinaendelea na kwamba serikali kamwe haitavivumilia.

Alisema ipo haja kwa wananchi katika maeneo kunakofanyika vitendo hivyo, kushirikiana na serikali katika kupambana navyo.

"Niwapongeze wananchi wanaoishi ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi kwa kuonyesha uzalendo na kushirikiana na serikali katika kudhibiti uvuvi haramu hususani unaotumia mabomu ambao kwa mujibu wa taarifa ya Mkoa wa Lindi, uvuvi huo umedhibitiwa kwa asilimia 100 katika eneo hili," alisema Ndaki.

Akiwa katika kijiji hicho, Ndaki alizitaka kampuni zinazonunua zao la mwani, kuacha mara moja kuwadhulumu wakulima wa zao hilo kwa kutumia mizani zisizo sahihi.

Alisema wizara hiyo itaangalia utaratibu kwa kushirikiana na halmashauri kuwawezesha wakulima wa zao hilo kupitia vikundi vyao katika kutengeneza bidhaa badala ya kuuza kama malighafi ili wanufaike zaidi kujiongezea kipato.

Alisema ni wakati mwafaka ambao wakulima wanapaswa kunufaika na mazao ya kilimo chao badala ya kuendelea kunyonywa na walanguzi.



Wawakilishi wa vijana wa dhehebu la Singasinga Mkoa wa Dar es Salaam, wakitoa msaada wa vitu mbalimbali kwa watoto wa kituo cha kulelea yatima cha Al- Hidaya kilichopo Buguruni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wapigadebe stendi Njombe waonywa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi mkoani Njombe limepiga marufuku wapigadebe wa mabasi ya abiria katika stendi za abiria mkoani hapa kuacha kuwalaghai abiria na kupandisha nauli kinyume cha utaratibu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alitoa agizo hilo jana kwa wananchi hususan abiria wanaosafiri kipindi cha Sikukuu ya Krimasi, huku akiwataka kutoa taarifa kwa askari pale wanapofanyiwa vitendo hivyo ili hatua zichukuliwe mara moja.

Alisema abiria atakayebughudhiwa na mpigadebe au kunyanyaswa wakati akisafiri, asisite kufikisha malalamiko yake kwa askari wanaokuwa ndani ya stendi, ili kushirikiana na maofisa wa Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini (LATRA) ili hatua zichukuliwe.

"Na ninyi abiria mchangamke, abiria unapokatiwa tiketi basi hulioni uwe makini. Kuna watu wanakatiwa tiketi halafu basi halionekani na unajikuta inafika mpaka usiku matokeo yake inakuwa kesi ya polisi na abiria. Unakuta hata yule aliyemkatia tiketi hajulikani alipo," alisema Issah.

Pia aliwataka wapigadebe wanaowalaghai abiria kwenye vituo vya mabasi kuacha tabia hiyo mara moja ikiwamo abiria wenyewe kutumia askari wa jeshi hilo kuwafichua watu wa namna hiyo.

Kuhusu jeshi lililovyojipanga kudhibiti uhalifu wakati wa sikukuu, Kamanda Issah alisema wameona kuna maeneo mengi yamekuwa yakikabiliwa na uvunjaji ikiwamo Makambako na Njombe, hivyo jeshi linaendesha doria ya usiku na mchana kudhibiti wizi wa namna hiyo.

"Njombe na Makambako haya ni maeneo kwa kweli na sisi tumejipanga katika kudhibiti ili uvunjani usitokee na sasa hivi doria za mchana na usiku zinafanyika na tunajitahidi kuwakamata watu wengi sana hususani tunaowakamata ni pamoja na wale wanaofanya utapeli mkubwa," alisema.

Wakati huo huo, Kamanda Issah aliwaonya watu watakaotumia sherehe ya Krismasi kupiga muziki kwa sauti ya juu ambao utasababisha bughudha kwa wengine, huku akisema hatua kali zitachukuliwa dhidi ya watu hao kwa kuwa sheria bado zinafanya kazi.

## PSSSF yahakiki wastaafu, wategemezi

**Na Richard Makore,** MWANZA

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) Mkoa wa Mwanza, umeendelea kufanya uhakiki wa wastaafu na wategemezi wanaopokea mafao yao, ili kuondokana na udanganyifu unaoweza kufanywa na baadhi ya watu.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jijini Mwanza jana, Kaimu Meneja wa PSSSF Mkoa wa Mwanza, Happiness Manyenye, alisema uhakiki huo hufanyika mara moja kwa mwaka.

Manyenye alisema uhakiki huo unafanyika katika wilaya zote za mkoa wa Mwanza na kila mstaafu anatakiwa kufika huko na picha moja, nakala ya kutambulisho cha taifa na nakala ya kadi ya benki.

Aidha, alisema kwa wastaafu ambao hawawezi kufika ofisini kutokana na ugonjwa wanaweza kufuatwa walipo na watumishi wa mfuko.

"Ili tuweze kumfuata mwanachama wetu ambaye hajiwezi, yeye mwenyewe au ndugu zake wanapaswa kutujulisha ili kumfikia mstaafu huyo," alisema

Meneja huyo alisema Mkoa wa Mwanza una zaidi ya wastaafu 5,000 wanaofanyiwa uhakiki na kwamba kila wiki wanahakiki wanachama kati ya 400 na 500.

## Wananchi waanzisha ujenzi zahanati

**Na Mwandishi Wetu,** RORYA

WANANCHI wilayani Rorya Mkoa wa Mara, wameanzisha mpango wa ujenzi wa zahanati katika kila kijiji kwa lengo la kuboresha huduma za afya.

Hayo yalibainisha juzi na Mbunge wa Rorya, Jafari Chege, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari.

Alisema mpango huo tayari umefanikisha ujenzi wa zahanati mpya 12 na ukarabati wa zahanati zingine 10 pamoja na ukamilishaji wa majengo kadhaa ya zahanati zilizokwama kwa kipindi kirefu.

Akizungumza katika hafla ya kuzindua ujenzi wa zahanati mpya katika eneo la Ngasaro, Mji Mdogo wa Shirati, Chege, alisema lengo ni kuboresha huduma za afya kwa kuhakikisha vifo vya mama na mtoto vinapungua.

Chege aliwataka wananchi wote walioko ndani na nje ya wilaya hiyo, kukamilisha mradi huo ndani ya muda wa miezi minne iliyopangwa.

Ili kuongeza kasi ya ujenzi huo, Chege alichangia mifuko 1,000 ya saruji na Sh. milioni 10 kwa ajili ya mafundi na kutaka ujenzi katika zahanati zote husika kuanza mara moja.

Katika ujenzi huo, wananchi wanachangia nguvu zao kama vile kufyatua matofali, kukusanya mawe na ufundi.

# TCC yatoa vifaa saidizi kwa wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Sigara Tanzania (TCC Plc) imetoa vifaa saidizi zaidi ya 800 kwa watu wanaoishi na ulemavu katika mikoa mitano, ikiwa ni sehemu ya programu yake maalumu ya huduma kwa jamii yake 'Tunaleta Mabadiliko Pamoja.'

Wilayani Ruangwa mkoani Lindi, TCC Plc imetoa vifaa saidizi zaidi ya 170 kwa watu wanaoishi na ulemavu.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya vifaa hivyo, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Albert Mwombeki, aliishukuru TCC Plc kwa kutoa msaada huo na kutoa wito kwa mashirika mengine na kampuni kuiga mfano huo.

"Msaada huu utawawezesha watu wenye ulemavu katika wilaya yetu na maeneo mengine yaliyonufaika na msaada huu kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii kwani itakuwa rahisi kwao kusogea kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine bila kuhitaji msaada mkubwa, jambo ambalo litatoa ahueni kwa familia zao na wanaowategemea," alisema na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kuunga mkono jitihada kama hizo za TCC Plc.

**Sasa tunaweza kufanya shughuli mbalimbali katika maeneo tofauti, tunaishukuru sana TCC na tunawaomba wasiishie hapo kwani bado msaada wao unahitajika.**

Mwenyekiti wa Chama cha Walemavu Tanzania (CHAWATA) Tawi la Ruangwa, Dorice Kamilos, alisema TCC Plc imekuwa mkombozi kwao kutokana na msaada iliowapa.

"Sasa tunaweza kufanya shughuli mbalimbali katika maeneo tofauti, tunaishukuru sana TCC na tunawaomba wasiishie hapo kwani bado msaada wao unahitajika," alisema.

Akizungumzia programu nzima, Meneja Uhusiano wa Serikali wa TCC Plc, Derick Stanley, alisema hadi sasa wametoa vifaa saidizi zaidi ya 800 katika mikoa mitano, Lindi ikiwa mojawapo.

"Hii inaendana na sera yetu ya huduma kwa jamii na pia tuliamua kungana na watu wanaoishi na ulemavu nchini katika mwezi huu, ambapo Siku ya Kimataifa ya Watu wenye ulemavu huadhimishwa Desemba 2 kwa maana hiyo mwezi wote huu tumeshirikiana nao katika mikoa mitano na kugawa vifaa saidizi," alisema.

Meneja huyo alisema mikoa iliyonufaika na misaada hiyo ni pamoja na Tabora ambapo waligawa magongo pea 100, fimbo nyeupe 100 na baiskeli 10 za magurudumu matatu,

Pia, Katavi walikotoa fimbo nyeupe 100, Rukwa baiskeli za magurudumu matatu 23, magongo pea 100 na fimbo nyeupe 15, Lindi magongo 100, fimbo nyeupe 100 na baiskeli za magurudumu matatu 28.

Alisema kuwa kwa mwaka jana peke yake, TCC iliwafikia zaidi ya watu 1,800 wanaoishi na ulemavu nchi nzima kupitia programu hiyo.

"Hakuna namna bora ya kumaliza mwaka kama hii ya kurudisha kwa jamii tunayoijali. Tunajivunia kwa sababu tunajua misaada hii itanufaisha familia zao pia na wategemezi wao kwani sasa wanufaika hawa wanaweza kushiriki katika shughuli za kujipatia kipato hivyo kwa pamoja tutaweza kupambana na umaskini," alisema.

Katika hatua nyingine, TCC plc imetoa msaada wa vyerehani kwa vikundi viwili vya wanawake vijulikanavyo kama Mvumweni na Wanambono vilivyopo katika vijiji vya Tae na Mbono wilayani Same.

Makabidhiano hayo yamefanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Same.



Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Edward Jotham, akisalimiana na mjane mke wa Hayati Edward Sokoine, Napono Sokoine, baada ya kuwasili nyumbani kwao jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## RC ashtukia ujenzi barabara kusuasua

**Na Saidi Hamdani,** LINDI

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, ameitaka Kampuni ya China Railway 15 (CR) iliyopewa kazi ya ujenzi wa barabara kutoka Nanganga wilayani Masasi mkoani Mtwara hadi Ruangwa mkoani Lindi, kuharakisha utekelezaji wake ili kuendana na mkataba.

Zambi alitoa agizo hilo jana, alipotembelea Kijiji cha Nandagala ambako kampuni hiyo imeweka karakana ya kuhifadhi vifaa vya ujenzi na nyumba za kuishi watumishi wa mradi huo, akishtuka kuona mradi uko katika hatua za awali huku muda uliotengwa ukiwa umekwishapita.

Alisema imekuwa ni tabia kwa baadhi ya makandarasi kutumia muda mrefu katika kufanya maandalizi kiasi cha kupitisha muda na matokeo yake, mradi mzima unachelewa kukamilika kinyume cha mkataba.

Muda wa ujenzi wa kambi ya mkandarasi huyo ulitakiwa uwe kuanzia Agosti hadi Novemba 21 mwaka huu, lakini wakati kiongozi huyo anazuru kambini hapo, alikuta kazi hiyo imefikia asilimia 30 tu.

Msemaji wa Kampuni hiyo, Faida Malunde, alisema kutokamilika kwa ujenzi wa kambi hiyo kwa wakati kumechangiwa na serikali kuchelewa kuipatia malipo ya awali kampuni hiyo, madai ambayo yalipingwa na Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Lindi, Efatha Mlavi.

Mlavi alidai licha ya serikali kuchelewa kuipatia fedha kampuni hiyo, siyo sababu ya msingi kushindwa kuanza kazi kwa kuwa mkataba unamtaka mkandarasi kuwa na uwezo wa kuanza kazi bila kutegemea malipo ya awali.

Mkuu wa Mkoa alimkumbusha mkandarasi huyo kauli ya Rais John Magufuli alipofanya ziara wilayani huko Oktoba mwaka jana, kwamba asingependa mradi huo uchelewe kwa namna yoyote ile.

# RC Ndikilo awabana wakurugenzi halmashauri

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, amewataka wakurugenzi wote wa halmashauri za wilaya katika mkoa huo kuhakikisha wanafungua na kukarabati barabara zilizo chini yao, ili kurahisisha kila eneo kufikika kwa urahisi muda wote.

Ndikilo alitoa agizo hilo jana wakati wa kikao cha bodi ya barabara kilichofanyika mjini Kibaha na kuwahusisha viongozi mbalimbali wakiwamo wakuu wa wilaya, wakurugenzi, meneja wa Wakala wa Barabara (Tanroad) na viongozi wa mkoa huo.

Alisema zipo barabara ambazo hadi sasa hazijaingizwa kwenye mtandao wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) ambazo zinaelezwa zipo chini ya usimamizi wa wakurugenzi, hivyo wanatakiwa kuzifungua kuleta urahisi kupitika bila vikwazo.

Alisema kufunguliwa kwa barabara hizo kwenye halmashauri, kutarahisisha maeneo ya viwanda kufikika kwa urahisi na wakulima wakiwamo wa zao la korosho kusafirisha mazao yao bila usumbufu.

"Serikali inahimiza ujenzi wa viwanda na wadau wameitikia, lazima tuhakikishe tunawawekea mazingira mazuri kwa kujenga barabara ili zipitike na kuwaondolea kero wanaposafirisha bidhaa zao na malighafi kwenda viwandani," alisema.

Alitoa rai kwa watendaji kuanza kuratibu utekelezaji wa ahadi za miradi ya maendeleo zilizotolewa na Rais katika kila sekta mkoani mwake.

Mhandisi Mkuu wa Bodi ya Mfuko wa Barabara, Jacob Mukasa, alisema zipo kero wanazokumbana nazo katika barabara za mkoa huo ambazo ni pamoja na uvamizi wa hifadhi ya barabara, utupaji wa taka kwenye hifadhi za barabara na uzidishaji wa mizigo kwa magari yanayopita katika mkoa huo.

Katika kikao hicho, wajumbe kutoka Kibiti waliomba kutengewa bajeti kwa ajili ya matengenezo ya barabara inayoenda katika Bwawa la Nyerere ili kurahisisha usafirishaji wa vifaa na mizigo mingine inayopelekwa kwenye bwawa hilo.

# Mkuchika ataka haki Sekretarieti ya Ajira

**Na James Mwanamyoto,** MOROGORO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapteni mstaafu George Mkuchika, amewataka watumishi wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, kutekeleza majukumu yao kwa kuzingati maadili na uwajibikaji.

Amesema hiyo itasaidia kutenda haki kwa kila mwombaji wa ajira serikalini ambaye ana sifa za kupata kazi kwa mujibu wa nafasi husika zinazotangazwa na taasisi mbalimbali za umma.

Mkuchika alitoa rai hiyo wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kilichofanyika mjini Morogoro.

Aliwasisitiza watumishi hao kuendelea kuzingatia uadilifu, sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia utumishi wa umma nchini kwa kuwa kazi wanayoifanya ni nyeti na inagusa maisha ya watu, hivyo inahitaji watu waadilifu, wapenda haki na ambao ni mfano wa kuigwa na jamii kwa uadilifu.

**Ni muhimu watumishi wa Sekretarieti ya Ajira kuwahudumia wateja wao kwa lugha nzuri kwa kuwa ndiyo nyenzo muhimu katika utoaji wa ajira.**

Akizungumzia utoaji wa huduma kwa wateja, Mkuchika alisema ni muhimu watumishi wa Sekretarieti ya Ajira kuwahudumia wateja wao kwa lugha nzuri kwa kuwa ndiyo nyenzo muhimu katika utoaji wa ajira.

"Tumieni lugha nzuri na yenye staha kwa kuwasikiliza na kuwahudumia vizuri wateja wenu kwani nyie ndiyo lango kuu la kuingiza watu katika utumishi wa umma, hivyo mienendo yenu ndiyo picha ya aina ya watumishi watakaopatikana kwa ajili ya kuja kusimamia utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo inayofanywa na serikali," aliagiza.

Mkuchika pia aliwahimiza watumishi hao kufanya kazi kwa kushirikiana na waajiri kwa kuwa ni jukumu walilopewa la kuendesha mchakato wa ajira kwa niaba ya waajiri hivyo ni muhimu wakashirikiana kuhakikisha mchakato wa ajira unakwenda vizuri na kwa wakati na hatimaye kupata watumishi wenye sifa stahiki ambao watalisukuma gurudumu la maendeleo ya taifa kwa kasi zaidi.

Aliwataka watumishi wa sekretarieti hiyo kurahisisha mchakato wa ajira kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kuchuja waombaji wa kazi, ikiwa ni kuunga mkono jitihada za Rais kuhimiza matumizi ya TEHAMA.

Akizungumzia matumizi ya TEHAMA, Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Xavier Daudi, alisema mifumo ya TEHAMA imeiwezesha ofisi yake kudhibiti matumizi ya vyeti vya kughushi katika uendeshaji wa mchakato wa ajira serikalini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zenye dhamana katika sekta za elimu na mafunzo wakati wa uhakiki.

Daudi aliongeza kuwa, kupitia mifumo ya kiutendaji ya TEHAMA, wamewawezesha waombaji kazi kupata na kufuatilia taarifa za matangazo ya kazi kupitia teknolojia rahisi ya simu za kiganjani popote alipo mteja ikiwamo mitandao ya kijamii ambayo imewapunguzia adha wafuatiliaji wa fursa za ajira kwa kuwa taarifa zinawafakia popote walipo.

Kuhusu uadilifu, Daudi alisema Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imejiwekea malengo kuhakikisha wanaoajiriwa katika taasisi za umma, wanakuwa na sifa ya uadilifu na uwajibikaji.




Naibu Gavana wa Benki Kuu, Dk. Benard Kibese (kushoto), akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Letshego Bank, Andrew Tarimo, wakifungua pazia kuzindua huduma ya mfumo wa malipo kupitia kadi ya Visa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukimwona mtoto huyu, toa taarifa

**Na Mwandishi Wetu**

MTOTO Fatuma Mweta (pichani), amepotea katika mazingira ya kutatanisha nyumbani kwa baba yake mdogo, eneo la Kibamba jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa baba yake mdogo, Cyprian Munish, Fatuma (13), aliondoka nyumbani Desemba 16 mwaka huu majira ya saa 3:30 usiku.

Alisema siku hiyo aliondoka pasipo kumuaga mtu yeyote, akidaiwa kumdanganya dada wa kazi kwamba anakwenda kuanua nguo nje.

Mushi alidai kuwa Fatuma hakwenda kuanua nguo, lakini aliondoka na hakurudi nyumbani.

Baba mdogo wa Fatuma alisema ameshatoa taarifa Kituo cha Polisi Gogoni na kuandikiwa namba ya jalada la polisi ***KAIR\RB\13108\2020.***

Alisema mtu yeyote atakayemwona mtoto huyo, atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho jirani au apige simu ***0715 540530*** au ***0747 636300***.



# Mwekezaji aahidi ajira 400

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MWEKEZAJI wa kiwanda cha kuchakata samaki mkoani Rukwa, Alpha Nondo, ameuomba uongozi wa mkoa huo kumtengenezea mazingira mazuri ya kuwekeza, ili atoe ajira kwa watu 400 na kumuunga mkono Rais John Magufuli katika ujenzi wa uchumi wa Tanzania.

Akizungumza na wakati wa uzunduzi wa Siku ya Ulaji Samaki mkoani hapa jana, Nondo alisema kuwa kupitia kampuni yake ya Alpha Tanganyika Flavor, ameamua kujenga kiwanda hicho mkoani hapa baada ya Rais Magufuli kuhamasisha wawekezaji kwenda kuwekeza Rukwa.

Alisema kuwa Novemba mwaka jana, Rais Magufuli akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Rukwa, alitoa wito kwa wawekezaji wa nje na ndani ya nchi kwenda kuwekeza mkoani Rukwa kwa kuwa kuna fursa nyingi za uwekezaji.

Nondo alisema kupitia wito huo, aliiona fursa katika Ziwa Tanganyika ndipo akaamua kuwekeza kiwanda hicho ambacho anakusudia kutoa ajira kwa vijana 400 ili iwe shukrani zake kwa Rais Magufuli sambamba na kufungua biashara ya samaki kimataifa.

Mkurugenzi huyo wa kiwanda cha kuchakata samaki, alisema anachohitaji ni serikali kutengeneza mazingira rafiki ili aanze uzalishaji na kutoa ajira kwa wakazi wa mkoa huo.

Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, ambaye alikuwa akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Dk. Halfan Haule, alimhakikishia mwekezaji huyo kuwa serikali ya awamu ya tano inawapenda wawekezaji ndiyo maana inawaita kuwekeza mkoani humo ili kukuza uchumi wa mkoa na kutoa ajira.

**Novemba mwaka jana, Rais Magufuli akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Rukwa, alitoa wito kwa wawekezaji wa nje na ndani ya nchi kwenda kuwekeza mkoani Rukwa kwa kuwa kuna fursa nyingi za uwekezaji.**

Mbunge viti maalumu CCM ajitutumua, adai Ukurasa 13




siasa

JUMATANO DESEMBA 23, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 14

PIERRE BUYOYA 1949 – 2020

# Azaki A/Mashariki zinataka raha 2021, zinalia madola 'yaziminya'

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

KATIKA jitihada za kuendeleza uhusiano mwema baina ya dola na wananchi, asasi za kiraia za Afrika Mashariki, zinashauri serikali za mataifa hayo, kuwapa uhuru na nafasi raia kufanya mambo mema wanayokusudia kupitia mashirika yao.

Wanazungumzia nafasi ya mashirika ya kiraia yanayojumuisha wananchi mbalimbali kama wanawake, walimu, wanahabari, madaktari, wabunge, wenye ulemavu na wafanyabiashara ambao ndiyo wana azaki, wakisema kikatiba wana nafasi na ni sehemu ya jamii.

"Uwapo wa azaki ni muhimu kwa vile ni uongozi ulioko kati ya utawala wa dola wenye serikali, mahakama na bunge, wakati mashirika ya kiraia hutumia taratibu za mila na misingi waliojiwekea," anasema Dk. Azaveli Lwaitama, mhadhiri mbobezi masuala ya filosofia na uongozi.

Akizungumza kwenye mkutano wa azaki za Afrika Mashariki kutafakari nafasi ya taasisi hizo, uliomalizika jijini Arusha mwishoni mwa wiki mhadhiri huyo wa zamani wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anasema;

"Taratibu na desturi zinatawala kwenye asasi za kirai. Watu wanakubaliana kutoa maoni, kushirikiana kama walimu, wafanyakazi, wakulima, madaktari na wauguzi. Hawatumii polisi wala magereza, wala mahakama. Ingefaa nafasi au uwanja uwe mpana na wa kutosha kuendeleza harakati hizo za kijamii."

Katika kusanyiko hilo mashirika ya kiraia yanaeleza kuwa serikali za mataifa yao zinazibana na kukwamishwa kufanya kazi kwenye 'uwanja' wake, wanaoamini uko kikatiba.

Wanasema ndani ya katiba za nchi hizo kuna uwanja wa azaki (raia) unaotoa haki kama ile ya uhuru wa maoni, kuamini dini atakayo, kushirikiana na wengine, haki ya kufanya kazi, kupiga kura, kuishi na kulindwa na serikali.

Alisema, mashirika hayo yanaiona hatua ya kukosa uhusiano wa kirafiki baina yao na dola unasababisha azaki kuwa wanyonge na kushindwa kushirikiana na serikali, jambo ambalo wanahisi linaweza kuwa na athari kwa jamii na umma ambao wanauhudumia.




Wadau wa azaki wakitafakari uwanja wao na namna bora ya kushirikiana na dola hivi karibuni jijini Arusha. Anayezungumza ni Nafula Wafula kutoka Kenya. PICHA: MWANDISHI WETU

Dk. Lweitama, mjumbe wa Bodi ya Shirika la Action Aid Tanzania, waandaaji wa mkutano huo, anasema azaki zinakubaliana na uwezo na uwapo wa serikali na ina sehemu yake, lakini haipendezi kuingilia kwenye kila kitu.

"Mashirika ya kiraia yana nafasi yake, yana umuhimu kuishauri serikali kikamilifu na hasa kwenye kuikumbusha kutimiza yale raia waliyoituma. Raia wanahitaji maji, kukomesha rushwa, elimu bora na afya..." anaongeza.

Washirika hao kutoka Kenya, Uganda, Tanzania na Rwanda, wanaeleza kuwa serikali inatakiwa kuruhusu uwapo wa azaki na kushirikiana nazo kwa vile si wapinzani wala hazina nia ya kuichukua dola.

Washirika hao wanapenda kuona Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo serikali zinaziona azaki kama washirika na si maadui ambao wanaisaidia kutoa huduma kwa jamii na kuiamsha isilale au kubweteka na wakati wote ifanye kazi umma ulizowatuma.

Baadhi ya mambo yanayoibuliwa na wadau hao kutoka Uganda, Kenya, Rwanda na Tanzania ni kufutwa kwa baadhi ya mashirika ya kijamii kwa sababu mbalimbali.

Wawakilishi kutoka nchini Uganda wanasema kuanzia mwaka jana baadhi ya mashirika takribani 10,000 yamefutwa kwa maelezo kuwa ni mawakala wa mabepari likiwamo linalotetea haki za wanawake.

Kwa upande wa wanahabari wanaeleza kuwa serikali yao ilifuta ithibati na kuwaagiza kujisajili upya, wakati waandishi wa habari wa kigeni wamekatazwa kuripoti uchaguzi mkuu wa Januari mwaka 2021. Hatua hizo zikichukuliwa mwezi huu.

Aidha, baadhi ya wadau kutoka Kusini mwa Afrika, wanadai kuwa azaki zimebinywa na kunyimwa 'uwanja' wake baada ya dola kukataza kuwasiliana na mabalozi wote wa kigeni walioko nchini humo.

Wanaona ni muhimu kuzikumbusha serikali kuwa taasisi hizo si maadui kwa vile ni sehemu ya wadau wanaotekeleza jukumu la kuwaletea wananchi maendeleo.

Washiriki hao wanaamini kuwa japo ni makundi yenye sura mbalimbali, lakini ndiyo raia wakihusisha watumishi wa umma kwenye vyama vya wafanyakazi, ni wawekezaji kwenye sekta binafsi, wakulima, wenye ulemavu na viongozi wa dini ambao wanahitaji kuwa na nafasi na kutoa maoni yao kuishauri, kuisaidia na kushirikiana na serikali zao.

Washiriki hao wanataka majadiliano baina yao na serikali yaendelea na malumbano yaishe na isiwaone raia wake kama wapinzani, wala mawakala wanaoshirikiana na mabereru.

Na ili kuendeleza uhusiano ni vyema kukutana na kujadiliana kwa lengo la kuwezesha kila mmoja kutimiza wajibu wake.

Aidha, azaki zinakumbushana kuwa ni wakati wa kuwajibika na kuendeleza utumishi mwema kwa upande wao hata kabla ya kuikosoa serikali na wadau wengine.

Mwakilishi kutoka taasisi za Uganda anakumbusha kuwa azaki zinahitaji kuwa na uadilifu, kuzingatia sheria na taratibu, kuwajibika kwa misingi ya katiba zake wakati zikielekeza dola na serikali kurekebisha upungufu wake.

Wadau wanasisitiza kuwa dola na azaki zinahitajiana kwa vile wote wamelenga kuwafikia wananchi kuwapa huduma kwa kusaidia kila mmoja akitimiza wajibu wake.

Mwakilishi kutoka Kenya, Nafula Wafula, anasema kinachotakiwa baina ya serikali na mashirika ya umma ni uhusiano wa kutegemeana (symbiosis), unaoongeza uwajibikaji, uwanja wa kuzungumzia utoaji zaidi wa haki za raia kisiasa, uchumi na huduma za kijamii.

"Tunachohitaji ni kuona kuwa huduma na haki muhimu za raia zinapatikana na kuwa mataifa yenye watu wenye furaha na utulivu," anasema.

# Kauli 'maendeleo hayana chama'...

## •Inavyoanza kutafsiriwa Nachingwea



Mbunge wa Nachingwea, Dk. Amandus Chinguile, akitoa neno kwenye mahafali ya darasa la saba ya Shule ya Msingi Silvernach, alipokuwa jimboni mwake wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Sabato Kasika**

'MAENDELEO hayana chama', ni kauli ambayo Rais John Magufuli, amekuwa akiirudia mara kwa mara katika hotuba zake, kwa kuwa wananchi wakibaguana kwa itikadi za vyama hawawezi kuungana kujiletea maendeleo.

Kutokana na umuhimu wa kauli hiyo, mbunge mpya wa Nachingwea, Dk. Amandus Chinguile, anasema anaichukulia kwa uzito na uhalisia na ameanza kuifanyia kazi jimboni mwake, ili wananchi waungane kuleta maendeleo na kujiondolea umaskini.

Katika mazungumzo yake na Nipashe hivi karibuni, mbunge huyo ambaye kitaaluma ni daktari wa binadamu, anasema, aliapa kuwatumikia wananchi wote wa Nachingwea bila ubaguzi, na kwamba madai ya yupi alimpa kura kwa vile yeye ni mbunge wa wote.

"Uchaguzi umepita, sasa ni wakati wa kuangalia habari za maendeleo lakini ikumbukwe kuwa hayana chama na ninaamini kuwa wananchi wa Nachingwea ndiyo walionichagua kuwa mbunge wao," anasema Dk. Chinguile.

Kiongozi huyo anasema, moja ya viti ambavyo Rais Magufuli amekuwa akihimiza ni maendeleo kutokuwa na chama wala kabila au mipaka, hivyo wabunge ni muhimu kuendelea kuhimiza hilo majimboni mwao.

"Binafsi nimeshaanza kazi hiyo ya kuwaambia wananchi wangu wa Nachingwea kuwa wamoja bila kujali itikadi za vyama, ili kujiletea maendeleo ambayo kila mmoja anayahitaji. Nimewaomba madiwani nao wahimize hilo kwenye kata zao," anasema.

Anaeleza kuwa umoja ni nguvu, hivyo wananchi hawana budi kuungana katika shughuli mbalimbali za maendeleo kwa vile uchaguzi umekwisha na sasa ni kusonga mbele wakisubiri mwingine mwaka 2025 baada ya miaka mitano ijayo.

> "Binafsi nimeshaanza kazi hiyo ya kuwaambia wananchi wangu wa Nachingwea kuwa wamoja bila kujali itikadi za vyama, ili kujiletea maendeleo ambayo kila mmoja anayahitaji. Nimewaomba madiwani nao wahimize hilo kwenye kata zao," anasema.

**AANZA KAMPENI**

Mbunge huyo anasema, kaulimbiu ya 'maendeleo hayana chama' ndiyo kampeni yake anayoendelea nayo awapo jimboni, na amekuwa akikutana na makundi mbalimbali ya wananchi kwa nyakati mbalimbali na kuzungumzia hilo.

"Kwa mfano, Desemba 18 mwaka huu nilifanya kikao na baraza la wazee wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Nachingwea na kuwaeleza jambo hilo kwamba maendeleo hayabagui chama," anasema.

Anasema, alikutana na baraza hilo kuomba wazee kumpa ushirikiano na kumshauri ili aweze kufikia malengo yake kwa wakati, hasa kushirikiana na wananchi ili kuleta maendeleo ya jimbo lao.

"Mimi ni mtoto wao nilijikabidhi mikononi mwao ili twende tufanye kazi kwa pamoja bila kujali itikadi za vyama, kwani maendeleo hayana chama na huo ni msisitizo wangu kama ambavyo Rais Magufuli ameeleza kwenye hotuba zake na wakati wa mikutano," anasema Dk Chinguile.

Anasema, wana CCM na wa vyama vingine wale wasio na vyama, hawana budi kuungana na kuweka mikakati ya pamoja kuhakikisha Nachingwea inazidi kupiga hatua kwenda mbele.

Mbunge Chinguile anasema, si hao tu bali kila akipokuwa jimbo huwa anatambelea hata vikundi mbalimbali vikiwamo vya wajasiriamali na wadau wa siasa na kuelezea msimamo wake huo unaolenga kuwaunganisha wana Nachingwea.

"Kama nilivyoeleza awali, niliapa kuwatumikia wananchi wote bila ubaguzi na sina kumbukumbu ya nani alinipigia kura, kwani mimi ni mbunge wa watu wote wa Jimbo la Nachingwea," anasema.

**VIPAUMBELE**

Anasema kama mbunge ana vipaumbele vyake jimboni ikiwamo huduma za jamii ikiwamo afya, maji na nyingine ambazo atashirikiana na viongozi wengine kuzitafutia ufumbuzi.

Lakini, yote hayo ninaweza kufanikiwa kwa ushirikiano na wananchi wote wa Nachingwea bila itikadi za vyama, ndio maana msisitizo wangu uko hapo kama ambavyo serikali inahimiza," anasema Dk. Chinguile.

Anaeleza kuwa Nachingwea kama yalivyo maeneo mengine ya nchi, ikiwamo uhaba wa madarasa, zahanati na vituo vya afya, na kwamba matatizo hayo yanatakiwa kutatuliwa kwa ushirikiano.

"Hata katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM wa 2020, imeainisha vipaumbele sita vitakavyotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo ikiwamo kulinda na kuimarisha misingi ya utu," anasema.

Anavitaja vingine kuwa ni usawa haki na uongozi bora ili kudumisha amani, umoja na mshikamano wa taifa, kukuza uchumi wa kisasa, ujumuishi na ushindani uliojengwa katika msingi wa viwanda, huduma za kiuchumi na miundombinu wezeshi.

Mbali na hivyo, anasema, ni kuleta mageuzi ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwa na uhakika wa chakula wakati wote na kuchangia kikamilifu maendeleo ya uchumi, kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, maji, umeme na makazi vijijini na mijini.

Vingine vinavyotajwa na chama hicho, ni kuchochea matumizi ya utafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu kama nyenzo ya maendeleo ya haraka ya kijamii na kiuchumi na kutengeneza ajira milioni nane.

"Vipaumbele hivyo vya chama na vyangu jimboni vinatakiwa kufanyiwa kazi kwa umoja, lakini pia kama Watanzania tunapaswa kuungana katika kutekeleza vipaumbele sita vya CCM, kwani ndicho chama tawala," anasema.

Anasema, madiwani nao wanatakiwa kuacha siasa, kwa madai kwamba uchaguzi umekwisha na sasa ni kazi tu ya kuleta maendeleo kwa kushirikiana na wananchi wote wenye vyama na wasio na vyama.

# Mbunge viti maalumu CCM ajitutumua, adai

## •Fedha si mali harakati za ubunge



Angelina Adam Malembeka, akimkabidhi pikipiki sheha wa Matemwe Kusini, Vuai Faraja Mcha, kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kazi za kuwahudumia wananchi.

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAPO wanaoamini kuwa fedha ni moja ya vikwazo vikubwa kwa wanawake kupata nafasi za uongozi hasa wa kisiasa, lakini Angelina Adam Malembeka, mbunge wa viti maalumu (wanawake) Mkoa wa Kaskazini Unguja hakubaliani na hilo.

Akizungumza na Nipashe, anasema kilichomwezesha kuibuka mshindi katika uchaguzi wa mwaka huu ni kujiamini na kuwa karibu na wananchi.

"Wapo wanaosema fedha ni msingi mkuu wa kupata uongozi, lakini mimi nasema sivyo. Wapo waliokuwa na pesa lakini hawakupata nafasi kwa kukataliwa na wajumbe hadi na wananchi kwa sababu wapigakura wanafahamu yupi kiongozi anayewafaa na anayetumia fedha kama fimbo," anakumbusha.

Akiwa na nia ya kusaidia juhudi za kuleta maendeleo mbunge huyo anaahidi kuwa atawatumikia wanawake, watoto na jamii ili kulinda utu, heshima ya mwanamke na mtoto na kuendeleza mustakabali mwema wa taifa.

Angelina anayetetea nafasi ya ubunge wa viti maalum katika mkoa huo kipindi cha pili kwa tiketi ya CCM, anasema ili upate mafanikio makubwa katika siasa ni lazima kukubali kujishusha chini kwa wananchi na kuwasikiliza kwa lengo na kuleta ufumbuzi.

"Katika kampeni zangu sijatoa hata senti bali ni ujasiri wangu na kuwa karibu na watu ambao ndiyo walioniwezesha kukubalika na wananchi pamoja na chama changu," anasema Angelina.

Kipindi cha miaka mitano iliyopita alifanya kazi na wanawake kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili makundi mbalimbali pamoja na wanaume, vijana na watoto, anasema.

Aidha, anasifu CCM kuwapa kipaumbele wanawake kuwania nafasi za uongozi kwa lengo la kufikia asilimia 50 kwa 50 katika vyombo vya maamuzi na kuondoa usindikazaji.

**VIPAUMBELE VYAKE**

Anataja kuimarisha upatikanaji, usambazaji majisafi na salama kwa wananchi kuwa ni mojawapo na kwa ujumla kuwatumikia wananchi wa mkoa wa Kaskazini Unguja.

> "Nakusudia kufuatilia zaidi miradi ya kinamama wajasiriamali kuanzia vikundi hadi mtu mmoja kwa lengo la kuona wanawake wanajikomboa kiuchumi na kupiga hatua kimaendeleo." Anasema mbunge huyo.

Anataja maji kwasababu katika baadhi ya maeneo mfumo wa usambazaji umeharibika hivyo kuwasumbua wananchi hasa wanawake ambao ndio wahusika wakuu kwenye huduma hiyo.

Angelina anatarajia kusimamia usambazaji wa maji na ujenzi wa visima, ili kupunguza tatizo sugu na kero ya maji vijijini.

"Nakusudia kufuatilia zaidi miradi ya kinamama wajasiriamali kuanzia vikundi hadi mtu mmoja kwa lengo la kuona wanawake wanajikomboa kiuchumi na kupiga hatua kimaendeleo." Anasema mbunge huyo.

**AWAMU YA KWANZA**

Anasema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ameifanyia kazi kubwa miradi ya wajasiriamali wanawake ingawa kuna kazi zaidi ili kupata mafanikio.

"Nimesaidia wajasiriamali wadogo katika vikundi mbalimbali vya wanawake ninaendelea sijakata tamaa nitawawezesha tena. Nia yangu ni kuona wanawake wanajikomboa kiuchumi na kuondokana na hali ya utegemezi," anasema.

Aidha, anasema atajikita zaidi katika kuimarisha huduma za afya kwa wajawazito na watoto, ili wajifungulie katika vituo vya huduma za afya kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

Anakusudia kuunga mkono juhudi za serikali kuu ikiwamo kuzipatia hospitali vitanda na vifaa vingine hatua ambayo italeta faraja kwa kinamama na kupunguza mazoea ya kupenda kujifungulia nyumbani na kuhamasika kuwahi hospitalini.

Angelina anasema tayari ameanza kuwafikia wananchi kwa kukabidhi pikipiki 12 kwa viongozi wa shehia (viongozi wa vijiji) masheha, ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao na kufuatilia maendeleo sehemu za kazi na hasa vijijini kusikokuwa na miundombinu madhubuti.

Anasema kazi ya masheha ni kubwa ambayo inahitaji usafiri wakati wa kutembelea maeneo mbalimbali na kukusanya taarifa muhimu za maendeleo kwa wananchi.

Anaeleza kuwa tatizo la uharibifu wa mazingira ni kubwa na anashirikiana na wadau wengine kuhakikisha kuwa misitu inalindwa na kutunzwa na sasa amewapatia majiko ya gesi 130 baadhi ya wanawake wa mkoa huo.

"Tunalenga kupunguza ukataji wa miti na uharibifu wa misitu kwa ajili ya matumizi ya kuni za kupikia," anasema na kuongeza kuwa anachukua hatua hiyo pia kwa ajili ya kuwapunguzia mzigo mkubwa kinamama wanaotembea masafa marefu kutafuta kuni kwa matumizi ya nyumbani na kwenye biashara.

"Huu si wakati wa kufanya sherehe kusherehekea ushindi au kupata nafasi ya uongozi bali ni muda muafaka kwa wabunge na viongozi wengine kurudi majimboni kutatua kero za wapigakura kama alivyosema Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, kuwaagiza wabunge kurudi majimboni kutekeleza ahadi walizotoa wakati wa kampeni."

Anasema kusherehekea ushindi ni sawa na kuwaumiza wale ambao waligombea nafasi hiyo, lakini hawakufanikiwa na kwamba ni mambo yanayojenga chuki kwa wengine.

Aidha, anaunga mkono juhudi zinazochukuliwa hivi sasa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kutekeleza majukumu yake na kutangaza viti dhidi ya rushwa na ufisadi ambavyo vimekuwa chanzo cha kukwamisha maendeleo ya taifa.

Anasema uchumi wa Zanzibar unategemea utalii, kilimo kikiwamo cha karafuu, mwani, ujasiriamali, uvuvi na yote hayo anakusudia kuyapa nafasi kwa kushirkiana na wapigakura wake.


# PIERRE BUYOYA 1949 – 2020

## • Ana nyayo mauaji Rais Ndandaye
## • Mauti yamkuta akiisuluhisha Mali

**Na Ani Jozeni**

SIYO watu wengi duniani wamewahi kufikia viwango vya kutawala au kudhibiti mifumo ya nchi kama Meja Pierre Buyoya.

Alikuwa Rais wa Burundi kwa vipindi viwili tofauti ambaye amefariki wiki iliyopita akiwa na miaka 71, umri ambao viongozi wa ngazi za juu kisiasa ndiyo wanakuwa wakistaafu. Lakini alishatoka madarakani.




**UONGOZI KITAIFA**

Alikuwa mkuu wa nchi Burundi mara mbili katika ujana wake, Septemba 1987 hadi Julai 1993, halafu akapindua tena 1996 na kuondoka madarakani tena 2003. Wako watawala wengine Afrika waliosimamia nchi kijeshi kwa vipindi tofauti, kama marehemu, Jerry Rawlings wa Ghana na Rais mstaafu wa Nigeria, Olusegun Obasanjo. Ila Buyoya hakuwahi kutoa madaraka kwa ridhaa yake kwa kiongozi wa kiraia.

Jijini Nairobi, shirika la habari la Reuters la Uingereza, lilitangaza kuwa Buyoya ambaye alifanya mapinduzi ya kijeshi mara mbili na chini yake vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyochukua maisha ya watu zaidi ya 300,000 amefariki.

Ni baada ya hukumu miezi miwili iliyopita, Mahakama Kuu ya Burundi ilimtia hatiani kwa mauaji ya mrithi wake aliyechukua madaraka Julai 1993, Melchior Ndadaye, aliyeshinda uchaguzi huo. Licha ya hukumu kutoka Buyoya hakuwa nchini humo.

Inadaiwa Ndadaye aliuawa na wanajeshi kwa amri ya Buyoya aliyekuwa akigombea nafasi hiyo na ambaye licha ya kuondoka madarakani, alikuwa bado jeshi lilimtii.

Licha ya kuwa Buyoya mwishowe alihukumiwa kwa kuhusika au kuamuru kuuawa kwa Ndadaye, mkasa halisi wa alichokifanya hauko katika tukio hilo na siyo wengi kati ya wasomi walioelezea kilichotokea eneo la Maziwa Makuu katika miaka ya 1990 wameweza kufafanua suala hilo.

Unaweza kusema kuwa kuuawa kwa Ndadaye ambaye alikuwa hajafahamika Afrika, akiwa na miezi mitatu madarakani, ni kama bomu la atomiki ambalo waliotekeleza kazi hiyo hawakuwa na ufahamu wanachokifanya ni nini hasa. Walitazamia jeshi liendelee kutawala labda zitokee ghasia.

**ATHARI ZA MAUAJI**

Inafahamika kuwa kuuawa kwa Ndadaye kuliingiza Burundi katika vita vya kung'oa mizizi ya utawala wa kijeshi ila suala hilo halikueleweka kwa viongozi wengi wa Afrika.

Vikundi vya kupambana na vikosi vya jeshi vilivyokuwa vikimtii Buyoya hata kama hakuwa madarakani vilikuwa mara nyingi vinaonekana kuchelewesha kutia saini makubaliano ya kufanya uchaguzi mwingine.

Viongozi wanaharakati au wapiganaji kama hayati Pierre Nkurunziza ambaye alifariki miezi michache iliyopita, ikihofiwa kushambuliwa na virusi vya corona.

Hawakukubali kutia saini kuacha mapigano, bila kuunganisha kikamilifu jeshi, na hivyo kuuvunja nguvu ya kabila moja la taifa hilo -Watutsi.

**KIFO CHAKE**

Taarifa ya Reuters ilisema kuwa wakati wa kifo chake Buyoya alikuwa akiishi nchini Mali ambako alikuwa na kazi maalum ya Balozi wa Umoja wa Afrika nchini humo, kutafuta suluhu ya machafuko ya vipindi tofauti ambayo miaka ya hivi karibuni yamebadilika kuwa wimbi la mashambulio ya makundi ya yenye uhusiano wa karibu na waasi wa dola la ISIS.

Kuondoka nchini Burundi mwaka 2012 ilikuwa kuhofia kushtakiwa, mjadala ukiendelea nchini Burundi kuhusu kuwawajibisha waliohusika na kuchochea vita, kuuawa viongozi wa kiraia waliopita baada ya Nkurunziza na kutwaa madaraka kiraia mwaka 2005.

Reuters ilisema kuwa ofisa mmoja wa Hospitali ya Pasteur jijini Bamako, Mali alisema kuwa Buyoya alitibiwa hapo kwa muda mfupi kabla ya kuhamishiwa hospitali nyingine huko Paris, Ufaransa, bila kutoa maelezo zaidi.

Ni radio ya kimataifa ya Ufransa RFI jijini Paris iliyosema kuwa Buyoya aliambukizwa virusi vya corona akiwa nchini Mali na kuhamishiwa Paris baadaye siku hiyo.

Ndugu wa karibu na familia ya Buyoya alinukuliwa, akisema kuwa Buyoya alifariki wakati anahamishiwa Paris kuendelea na matibabu hayo.

Baadhi ya wachambuzi wa kimataifa wanasema alishika madaraka kwa muda mrefu nchini humo, licha ya kutawala kwa miaka 13 kama rais.

Alimpindua rais wa nchi hiyo, Meja Jean-Baptiste Bagaza, mwaka 1987 kwa sababu alikuwa amelikamata jeshi kwa miaka kadhaa, licha ya kuwa na umri wa miaka 38 wakati huo.

Na alipoondoka madarakani mwaka 1993 aliendelea kushikilia jeshi, akiamuru kuuawa Ndadaye na hali kuparaganyika zaidi kisiasa, akatwaa madaraka tena mwaka 1996 na kuondoka 2003 tena ni kwa sababu hakuwa na jinsi.

**VITA VISIVYOKOMA**

Kuuawa kwa Ndadaye miezi mitatu baada ya kuingia madarakani kulianzisha vita katika nchi tatu za Rwanda, Burundi na Congo na bado matokeo yake yapo.

Mataifa hayo hayajatulia kikamilifu, licha ya vuguvugu la vita kuanza nchini Burundi wakati huo, ni Rwanda iliyoanza kuwaka moto, kwani waliokuwa madarakani ambao ni kabila kubwa zaidi la Wahutu, waliokuwa wakipambana na jeshi lenye Watutsi kwa wingi zaidi likiongozwa na Paul Kagame.

Kiongozi huyo alitokea Uganda akiwa akiwa jeshini katika harakati za kuondoa utawala wa kijeshi wa majenerali Tito Okello na Oyite Ojok.

Mwaka 1986, Yoweri Museveni aliingia madarakani, huku vuguvugu hilo nalo kuparaganyika baadaye.

Wakuu wa vyombo vya usalama vya Rwanda, alipouawa Ndadaye katika taifa pacha la Burundi (wana jamii zinazofanana na Wahutu na Watutsi, na Watwa wachache) waliangaliana usoni, ili kupima kama wanaweza kuwaamini hao waliokuwa wakipambana nao.

Suala ni kama wakitwaa madaraka hawatakuwa sawa na wenzao wa Burundi, kuhakikisha kuwa Wahutu wanakandamizwa kama ilivyokuwa Burundi tangu mauaji ya kimbari ya mwaka 1972?

Ndiyo mzizi wa mauaji ya kimbari yaliyoanza usiku wa Aprili 6, 1994.

Miaka mitatu baadaye, kundi hilo likiwa linawafuatilia wapiganaji wa Kihutu waliohamia Congo kujipanga upya halafu kurudi kuendelea na mauaji, lilianzisha wimbi kuung'oa utawala wa hayati Mobutu Seseseko akiwa taabani na saratani, akafariki nchini Morocco.

Waliuondoa utawala wa Mobutu na hivyo kusababisha vita mpya, nchi za jirani zikizuia wimbi la utawala wa kifalme na ubaguzi wa Maziwa Makuu.





# Ndalichako ang'aka takwimu ujauzito

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amepiga marufuku maofisa elimu kutoa takwimu za mimba kwa wanafunzi wa kike, huku akisema takwimu alizo nazo zinaonyesha kuwa wanafunzi wa kiume ndio wanaongoza kwa kuacha masomo.

Aidha, Ndalichako amewataka maofisa hao kusimamia ubora wa elimu unaotolewa katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha maofisa elimu wa taaluma, michezo, utamaduni, elimu maalum na takwimu wanatimiza wajibu wao.

Prof. Ndalichako alisema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mkutano wa saba wa Chama cha Maofisa Elimu wa Mikoa na Wilaya (REDEOA) jijini Dodoma.

**Serikali ipo katika mpango wa kujenga shule ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya viziwi katika eneo la Lukuledi mkoani Mtwara.**

Alisema takwimu ambazo anazo zinaonyesha kuwa wanafunzi wa kiume wengi ndio wanaoacha masomo na kwenda kufanya biashara, lakini kila siku maofisa elimu wamekuwa wakitoa takwimu za mimba za wanafunzi wa kike.

"Naomba tuwaheshimu na kuwathamini watoto wa kike. Baadhi ya kauli zinazotolewa zinakuwa hazina afya na ni za udhalilishaji kwa sababu watoto wetu hata wale wanaopata ujauzito tuwaone kama binadamu. Wakati mwingine kauli zinazotolewa hazipendezi, hivyo niwaombe maofisa elimu, kuna takwimu za kutoa kila siku mimba tu inakuwa kama vile hakuna kitu kingine cha kusemea," alisema.

"Takwimu zangu zinanionyesha watoto wa kiume ndio wengi wanaoacha masomo na takwimu hizi zinatoka kwenu. Sasa kama zimechakachuliwa mmezileta ninyi hasa katika maeneo ambayo ni ya wavuvi na wafugaji. Unaona saa za shule wanauza kwenye mabasi wale kwani hamuwaoni?" Alihoji Ndalichako.

Prof. Ndalichako alisema sekta ya elimu inafanya kazi vizuri, lakini anataka wafanye vizuri zaidi ikiwa ni pamoja kuwasimamia maofisa elimu wote walioko katika maeneo yao kuhakikisha wanatenda kazi ambayo wanatakiwa kuifanya.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha inaboresha masomo yote yanayowajengea uwezo wanafunzi kwenye maisha yao ya kawaida kama masomo ya kilimo.

Pia alisema serikali imeishaagiza magari 184 kwa ajili ya maofisa elimu na ifikapo Januari 15, mwakani, yatakuwa yameshafika nchini.

Sambamba na hilo, aliwataka maofisa elimu hao kusimamia elimu maalum kwani ni kundi ambalo linahitaji kusaidiwa kwasababu lina watu wachache.

"Jambo lingine nawaomba tusimamie elimu maalum na ninaomba mjitume zaidi kwani bado kuna chagamoto zipo kuna baadhi ya wilaya zinafanya vizuri na zingine zinafanya vibaya. Wale wenye mahitaji maalum wanatakiwa kuangaliwa kwa jicho la kipekee," alisema.

Alisema serikali ipo katika mpango wa kujenga shule ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya viziwi katika eneo la Lukuledi mkoani Mtwara.

Katika hatua nyingine, Waziri Ndalichako alisema serikali imepata mkopo wa Sh. trilioni 1.2 kutoka Benki ya Dunia ambazo zitatumika kujenga shule mpya za sekondari 1,000 pamoja na shule za kidato cha tano na sita 26 kwa ajili ya masomo ya sayansi kwa watoto wa kike.

Mwenyekiti wa REDEOA, Germana Mung'aho, alisema baadhi ya changamoto wanazokabiliana nazo ni pamoja na ukosefu wa magari kwa maofisa elimu wilaya, upatikanaji wa vitabu vya ziada na kiada pamoja na uhaba wa walimu wa masomo ya kilimo.

## Walimu kuwezeshwa kupata mikopo nafuu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKATI walimu wakitaja changamoto inayowakabili kuwa ni riba kubwa za mikopo kwenye taasisi za fedha, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) imeahidi kuhakikisha inaendelea kubuni huduma nafuu za kifedha zitakazosaidia walimu kufikia malengo yao.

Akizungumza katika mkutano wa Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSSA), Meneja wa Benki ya NBC Mkoa wa Dodoma, Happiness Kizigira, alisema wanatoa huduma za bima za afya, magari na majengo na kwamba mtu anaweza kufanya vitu vyake vikaenda salama na inapotokea majanga kupata fidia.

Rais wa TAHOSSA, Frank Mahenge, alitaja changamoto zinazowakabili walimu ikwamo mikopo yenye riba kubwa inayopunguza ufanisi na kuwakosesha utulivu kazini.

Alitaja changamoto nyingine ni matukio ya kuungua kwa shule, maeneo ya shule kutopimwa, ukosefu wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wakuu wa shule na ukosefu wa usafiri hasa kwa shule za bweni.

"Jambo lingine ukosefu wa vyombo vya usafiri hasa kwa shule za bweni, lakini hivi karibuni tulipata changamoto ya baadhi ya shule kuungua moto na shule nyingi kutokuwa na uzio imara, hivyo kuhatarisha usalama wa watumishi na wanafunzi," alisema.

Changamoto hizo huenda zikawa fursa kwa NBC ambayo tayari ina huduma mbalimbali za elimu ikiwamo bima ya elimu, akaunti za shule pamoja na akaunti za wanafunzi pamoja na mikopo yenye riba nafuu.

"Tulitoa elimu kuwa kuna bima wanazoweza kukatia shule zao ili pindi majanga yanapotokea akaweza kurejeshewa jengo lake. Kwa hiyo mwitikio umekuwa mzuri sana na hatutaishia hapa tutatembea hadi katika shule hizo kuhakikisha kuwa kuwa walimu wanapata elimu hii," alisema.




Waziri wa Nchi (TAMISEMI), Selemani Jafo, akizungumza na Meneja wa Huduma kwa Wateja wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) Tawi la Dodoma, Anne Mwaisaka, wakati alipotembelea banda la benki hiyo, kwenye Mkutano wa Mwaka wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSA), uliofanyika jana, jijini Dodoma. Benki ya NBC ni mmoja wa wadhamini wa mkutano huo, utakaofanyika kwa siku tatu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ndugai akemea fikra potofu ajira

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewataka vijana kuacha fikra potofu ya kusubiri kuajiriwa serikalini badala yake watumie fursa zilizopo kuibua miradi itakayowainua kiuchumi.

Ndugai alisema hayo kwenye uzinduzi wa ibada maalumu iliyofanyika kwenye Kanisa la Kristo Mfalme Anglikana Chamwino, Dodoma kwa ajili ya kuwahamasisha Watanzania kuzipenda bidhaa zinazozalishwa nchini.

Akizungumza kwenye hafla hiyo mbele ya waumini kutoka madhehebu mbalimbali ya dini, alisema bado kuna baadhi ya vijana wanaendelea kukaa vijiweni kusubiri nafasi za ajira suala ambalo ni mtizamo hasi kwa hivi sasa.

Alisema hivi sasa kuna fursa nyingi ambazo zinazoweza kuwaingizia kipato ikiwamo ufugaji, kilimo cha zabibu na buastani za mboga badala ya kuendelea kukaa vijiweni.

"Kwa kweli inasikitisha kuona vijana hivi sasa wanashinda vijiweni na majumbani na simu zao kwa ajili ya kuchati kutafuta ajira na vitu ambavyo havina faida kwao, wakati muda huo wangeweza kushughulika na akili ya kuibua miradi mbalimbali ambayo ingewatoa kwenye umaskini," alisema Ndugai.

Spika Ndugai aliviomba viwanda vinavyozalisha bidhaa mbalimbali nchini, vihakikishe vinakuwa na bidhaa zenye ubora, ili Watanzania waendelee kujivunia na kuzipenda zaidi.

Alisema viwanda hivyo vikizalisha bidhaa zake kwa ubora Watanzania watathamini na kusaidia kukuza uchumi wake na ajira kuongezeka.

Awali, akizungumza na waandishi wa habari Mratibu wa Tukio hilo, Simon Gunju, alisema malengo ni kuwahamasisha Watanzania kuzipenda bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuimarisha uchumi na kukuza ajira.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Kenneth Yindi, aliomba serikali na taasisi mbalimbali za uzalishaji kutoa elimu kwa Watanzania juu ya umuhimu wa kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini.





# Waonywa utumiaji mbegu zisizo na ubora

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Udhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), imewaonya wakulima juu ya tabia ya kupanda mbegu zinazoingizwa nchini kinyemela kwa kuwa hizo zina madhara makubwa.

Maofisa wa taasisi hiyo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, walifanya ukaguzi wa kushtukiza mwishoni mwa wiki kwenye maghala ya kuhifadhia na maduka ya kuuzia mbegu hizo katika mikoa ya Mbeya na Songwe.

Ofisa Mfawidhi wa TOSCI Nyanda za Juu Kusini, Peter Nassari, alisema madhara ya wakulima kutumia mbegu zisizothibitishwa ubora ni makubwa kuliko serikali kukosa kodi ya uingizwaji wa mbegu hizo.

Alisema moja ya madhara hayo ni pamoja na matatizo ya kiafya na kuzorotesha mavuno kutokana na mbegu hizo kuzalishwa kulingana na hali ya hewa ya nchi husika.

Nassari alisema mbali na madhara kiafya na kwenye mavuno, pia uingizwaji wa mbegu hizo kinyemela una athari za kiuchumi kwa taifa kutokana na kukosa kodi. Alisema endapo uzalishaji utaporomoka kutokana na matumizi ya mbegu hizo pia uchumi utazorota.

**Mbegu zinazozalishwa nchini zina ubora wote, sisi kinachotusumbua ni ile kasumba ya watu kuamini kwamba kitu cha nje ni bora kuliko cha kwetu.**

"Sheria inataka mkulima atumie mbegu ambazo zimethibitishwa ubora na TOSCI. Sasa kitendo cha watu kuingiza mbegu na kuanza kuzitumia bila kuthibitishwa ni kosa. Lakini mbegu ambazo wanaingiza ni zile zile ambazo zinazalishwa hapa nchini," alisema na kuongeza:

"Mbegu zinazozalishwa nchini zina ubora wote, sisi kinachotusumbua ni ile kasumba ya watu kuamini kwamba kitu cha nje ni bora kuliko cha kwetu."

Naye Mdhibiti wa Ubora wa Mbegu kutoka taasisi hiyo, Salehe Kombo, aliwataka wakulima kuhakikisha mbegu wanazonunua zina nembo ya TOSCI ambayo inaashiria kuwa imethibitishwa ubora.

Aliwataka wafanyabiashara pia kuacha kuuza mbegu ambazo hazijathibitishwa na taasisi hiyo kwa maelezo kuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria na endapo watakamatwa kuna adhabu kali ambazo zimeainishwa.

Pia aliwataka wakulima kuhakikisha kila wanaponunua mbegu wapewe risiti na wazitunze, ili ikitokea madhara yoyote iwe rahisi kumsaidia kwa kufuatilia kule alikonunua.

"Ukinunua mbegu bila kuchukua risiti hata sisi hatuwezi kukusaidia endapo utapata matatizo. Lakini ukiwa na risiti inakuwa rahisi kujua mahali pa kuanzia," alisema Kombo.

Baadhi ya wazalishaji wa mbegu walisema kuna matatizo mbalimbali ambayo yamekuwa yakitokea ikiwamo mabadiliko ya hali ya hewa ambayo huwa yakitokea wakulima wanakuwa na walakini na mbegu zao.

Mmoja wa wazalishaji hao, Christopher Shimwela, alisema mbali na matatizo hayo hali ya hewa ambayo yaliwakumba wakulima mwaka kwa mvua kunyesha kupita kiasi, pia kuna tatizo la wadudu kushambulia mazao.



Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUKTA), Tumaini Nyamhokya, jana, alikata utepe kuashiria ufunguzi wa maboresho ya ujenzi wa jengo la utawala la Chuo cha Wafanyakazi Tanzania (OTTU) , ambalo limefikia asilimia 50. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Dk. Tulia awapa mbinu wahitimu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA wanaohitimu elimu ya juu, wametakiwa kuachana na dhana iliyoenea mitaani kwamba hakuna ajira na badala yake watumie elimu waliyoipata kutatua matatizo yaliyopo kwenye jamii inayowazunguka.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, wakati wa mahafali ya tano ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Katoliki Mbeya (CUCoM).

Alisema baadhi ya dhana hizo zina uhalisia na zingine ni uzushi, hivyo ni lazima wahitimu wawe na uamuzi wa kisomi.

Aliwataka vijana hao kwenda mitaani wakiwa na dhana ya kwenda kujiajiri kwa kuanzisha shughuli zao, ili wawaajiri na wengine huku akiwataka kutobweteka kutafuta ajira.

"Ukifika mtaani usije ukaangalia watangulizi wako kwamba wao wamekaa muda mrefu bila ajira. Wewe gangamala kutafuta ajira, huku ukiendelea kufanya shughuli zako za kukuingizia kipato na uajiri wengine," alisema Dk. Tulia.

Mkuu wa Chuo cha CUCoM, Prof. Romuald Haule, aliwataka wahitimu kwenda kuwa wazalendo wa nchi yao, ili jamii inufaike na elimu waliyopata.

Aliwataka kuhakikisha kila jambo wanalolifanya kuhakikisha wanafikiria nchi yao kwanza na siyo kuwa na maslahi yao binafsi na wakaisahau nchi yao.

"Ukienda kufanya chochote lazima ufikirie kwanza mama Tanzania. Nendeni mkafanye kazi kwa bidii, jitahidini kuzingatia maadili ya kazi yoyote ambayo mtakuwa mmeajiriwa," alisema Prof. Haule.

Aliwatahadharisha vijana hao kufanya mambo ambayo yatakidharirisha chuo hicho pamoja na wazazi wao na badala yake wanatakiwa wawe mabalozi wema wa chuo hicho.

Baadhi ya wahitimu walisema elimu waliyoipata chuoni hapo itawasaidia kujiajiri na kwamba hata wakiajiriwa bado watajishughulisha na kazi mbadala za kujiajiri ili kujipatia kipato mbadala.

## Mpango upatikanaji pembejeo wazinduliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau wa kilimo, imeanzisha mpango kabambe wa upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu ili kuinua sekta hiyo.

Mpango huo unajulikana kwa jina la 'Kilimo Akiba' ambao ni wa kielektroniki unaowaunganisha wakulima waliojiunga kwenye vikundi na taasisi za kifedha hasa benki. Kupitia mpango huo, wakulima wanajiwekea akiba kidogo kidogo kwa ajili ya kulipia pembejeo hizo.

Akizungumzia mpango huo juzi, Mkurugenzi wa Kilimo Akiba, Mahamoud Shoo, alisema waliubuni kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wadogo kuongeza uzalishaji na kuongeza ubora wa mazao.

Alisema walibaini kuwa wakulima wengi wanashindwa kuzalisha mazao yenye ubora kutokana na kushindwa kuzipata pembejeo hizo kwa wakati pamoja na baadhi yao kushindwa kumudu bei.

"Tuligundua kwamba wakulima wengi hawawezi kutunza fedha kwa ajili ya pembejeo ndiyo maana wengi huwa wanapata shida wakati wa kuhudumia mashamba yao, hivyo tumeamua kuanzisha mfumo huu rasmi ambao mkulima anajiwekea akiba kwenye benki," alisema Shoo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, alisema mpango huo una baraka za serikali, hivyo wananchi wasiogope kujiwekea akiba hiyo kwa maelezo kuwa itawasaidia kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Alisema kutokana na sekta ya kilimo kuwa kubwa, ni vigumu serikali peke yake kutatua matatizo yanaikabili ndiyo maana huwa inashirikiana na sekta binafsi zikiwamo taasisi za kifedha kuyatatua.

Ntuinika aliwataka wananchi kuendelea kujiunga kwenye vikundi ili wawe na sifa za kupata huduma kupitia mpango huo na kwamba lengo la serikali ni kuendelea kuisimamia kwa ukaribu sekta ya kilimo ambayo ndiyo inayosaidia upatikanaji wa chakula na malighafi za viwanda.

Mkuu wa Wilaya ya Momba mkoani Songwe, Juma Irando, aliishukuru serikali kwa kuanzisha mpango huo na kwamba umeanzia katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ndiyo inayoongoza kwa kilimo.



# Masheha wataka orodha wadaiwa sugu

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MASHEHA wa Wilaya ya Mjini, wamemwomba Waziri wa Ardhi, Maendeleo na Makazi kupitia Shirika la Nyumba kuwapatia orodha kamili za nyumba za serikali na umiliki wa nyumba hizo, ili kurahisisha utendaji wa kazi zao.

Wakizungumza jana katika kikao na Waziri wa Wizara hiyo, kilichofanyika mjini Zanzibar, walisema kupatiwa kwa hati hizo zitasaidia kuwajua wakazi wa nyumba hizo na wadaiwa sugu ambao wanaishi katika nyumba hizo.

Katika kufuatilia nyumba hizo, walisema wamebaini kuwa kuna changamoto nyingi ikiwamo mmiliki halali ambaye amepewa nyumba na serikali kukodisha.

**Ni vyema pia kufanyiwa marekebisho wa mkataba wa nyumba hizo.**

Sheha wa Miembeni, Ali Abdallah Kidemere, alisema ni vyema pia kufanyiwa marekebisho wa mkataba wa nyumba hizo.

"Katika nyumba hizi tumebaini watu wanaoishi ni tofauti na mikataba tuliyo nayo na wengine wanaishi bure bila kuchangia kodi zinazotolewa katika Shirika la Nyumba," alisema.

Hata hivyo, alisema watendaji wa Shirika la Nyumba hawaonani na masheha hadi wakiwa na shida zao ndipo huwatambua masheha hao.

Aidha, alisema kumekuwa na changamoto ya miundombinu mibovu ikiwamo karo jambo ambalo linafanya uwepo wa uchafu na kuzagaa kwa taka.

Naye Waziri wa Wizara hiyo, Riziki Pembe Juma, aliwahakikishia masheha hao kushirikiana nao ili kuhakikisha changamoto za nyumba hizo za maendeleo zinatatuliwa pamoja na wakazi kulipa madeni.

Alisema kumekuwapo na malalamiko mengi kwa wananchi wanaotafuta nyumba za serikali kutozwa kodi kubwa hali ambayo inawapa ugumu kuzipata nyumba hizo.

Sambamba na hayo, alikiri kuwapo kwa baadhi ya changamoto na kuahidi kuzitatua ili maendeleo ya nyumba hizo yafikiwe.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, akimsikiliza Ofisa wa Chumba cha Kuchakata Taarifa, Fatma Khatib, akimwelezea jinsi taarifa za waombaji pasi za kusafiria zinavyohakikiwa wakati wa ziara ya naibu waziri huyo, Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji, Zanzibar. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# Wapewa mchongo maonyesho bidhaa

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAJASIRIAMALI wametakiwa kutengeneza bidhaa zenye kiwango na kuzitumia fursa za maonyesho ya biashara kutangaza biashara zao na kujipatia kipato, ili kupunguza tatizo la ajira nchini.

Hayo yalielezwa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Viwanda, Juma Hassan Reli, wakati akizungumza katika ufungaji wa tamasha la tatu la maonyesho ya wajasiriamali katika kiwanja cha kufurahishia watoto Kariakoo Mjini Zanzibar.

Alisema fursa za maonyesho ya biashara kutawasaidia wajasiriamali kujitangaza na kujipatia wateja kutoka sehemu mbalimbali.

Alisema maonyesho ya biashara ni fursa muhimu kwa wajasiriamali ili kukuza soko la bidhaa zao na kuwapatia nafasi ya kukutana na wafanyabiashara wengine kubadilishana uzoefu ambao utaendeleza sekta ya biashara nchini.

"Ni vyema kuacha kufanya biashara kwa mazoea. Ningewaomba wajasiriamali wazitumie fursa za mafunzo, ili kupata taaluma na ujuzi wa kufanya biashara kisasa ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia," alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema elimu ya ujasiriamali na mafunzo ya biashara ni muhimu kwa mjasiriamali ambaye ana malengo ya kuinua biashara zake na kupiga hatua ya kimaendeleo.

Alisema hivi sasa wafanyabiashara wengi wanatumia teknolojia ya mawasiliano hasa kupitia mitandao ya kijamii ambayo hutumiwa na watu wengi katika kuzitangaza biashara zao ili kukuza soko la bidhaa zao.

Pia Katibu Mkuu huyo aliupongeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kwa kuandaa tamasha hilo ambalo linaenda sambamba na azma ya serikali ya kuwainua wafanyabiashara wadogo.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZSSF, Sabra Issa Machano, ameongeza muda wa maonyesho hayo hadi Desemba 26, mwaka huu, ikiwa ni kutekeleza maombi ya wajasiriamali walioshiriki katika maonesho hayo ya kutaka kuongezewa muda.

"Kwa uwezo nilio nao ninayaongeza muda maonyesho haya mpaka Desemba 26 na watu wataendelea kuingia bure katika viwanja hivi hadi tarehe niliyoisema," alisema mkurugenzi huyo.

Baadhi ya wajasiriamali walioshiriki katika tamasha hilo waliushukuru uongozi wa ZSSF kwa kuwaongezea muda na kuwaomba kufanyika kwa tamasha hilo zaidi ya mara tatu kwa mwaka.

Tamasha hilo la tatu la maonyesho ya wajasiriamali limedhaminiwa na mashirika na taasisi mbalimbali zikiwamo CRDB, NMB, NHIF, TPB na Vigor Group of Companies.

# Wizara yakabidhiwa chuo cha ufundi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imetiliana saini makabidhiano ya Chuo cha Mafunzo ya Amali kilichoko Daya kisiwani Pemba baada ya kukamilika kujengwa.

Akizungumza baada ya makabidhiano hayo jana, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Idrissa Muslim Hija, alisema kutokana na kukamilika kwa ujenzi wa chuo hicho, kuna haja ya kuanza kutumika ili wananchi kunufaika katika kupata taaluma.

Idrissa alisema matarajio yao ni kuanza kutoa mafunzo ndani ya chuo hicho Februari, mwakani pamoja na chuo cha amali kilichoko Makunduchi.

Aidha, Dk. Idrissa aliutaka uongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kuweka utaratibu maalumu na kuandaa mazingira kwa ajili ya wanafunzi kuanza kujiandikisha katika chuo hicho, ili kuanza masomo ifikapo Februari.

Katibu Mkuu aliishukuru kampuni ya ZECCON kutoka Tanzania Bara kwa kukamilisha kazi hiyo kwa kiwango kinachoridhisha na kuwapongeza wote walioosimamia ujenzi huo tangu mwanzo hadi kukabidhiwa.

Mkandarasi wa ujenzi, Ali Mbarouk Juma, aliishukuru wizara kwa kumwamini na kumpatia kazi hiyo ambayo tayari imekamilika katika kiwango kilichotakiwa.

Pia alisema atayafanyia kazi yale yote ambayo wizara imemwomba kuyakamilisha na kuahidi kufanya hivyo bila ya malipo yoyote.

Naye mshauri mwelekezi wa mradi huo, Mohammed Suleiman Nassor, aliipongeza wizara kwa ushirikiano mkubwa uliowapatia kwa kipindi chote cha ujenzi na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano wao kadri watakapohitajika.

Makabidhiano hayo yamefanyika baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kampuni ya ZECCON kutoka Tanzania Bara kwa kushirikiana na mshauri elekezi wa mradi huo.

## HABARI KIMATAIFA

# Ivory Coast yaanza kutafuta suluhu ya kisiasa

**Abidjan, IVORY COAST**

SERIKALI na upinzani nchini Ivory Coast, wameanza mazungumzo kumaliza mvutano wa kisiasa nchini humo, baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba, mwaka huu.

Mazungumzo hayo yameanza kwa kuangazia mageuzi ndani ya Tume ya Uchaguzi kuelekea uchaguzi wa wabunge, utakaofanyika mapema mwaka 2021.

Waziri wa maridhiano ya kitaifa, Kouadio Konan Bertin, alisema kuanza kwa mazungumzo hayo, kunadhihirisha wazi pande zote zinahitaji amani.

Taifa hilo la Afrika Magharibi, limekuwa katika mvutano wa kisiasa tangu Agosti, mwaka huu, wakati Rais Alassane Ouattara, kutangaza kuwania urais kwa muhula wa tatu, hatua ambayo ilipingwa vikali na wanasiasa wa upinzani waliosema ni ukiukwaji wa Katiba.

Vurugu za kisiasa zilishuhudiwa kati ya wafuasi wa upinzani na maofisa wa usalama na kusababisha vifo vya watu 85 na wengine zaidi ya 500 kujeruhiwa.

Licha ya pingamizi hizo, Rais Ouattara aliwania tena na kuibuka mshindi katika uchaguzi huo uliofanyika Oktoba na baada ya kuapishwa, kukutana na kiongozi wa upinzani, Konan Bedie.

Rais Outtara aliomba kufanyika kwa mazungumzo kati ya serikali na upinzani.

***RFI***




Maofisa wa usalama wakidhibiti eneo lililofungwa katika Bandari ya Dover, Uingereza. Nchi za Umoja wa Ulaya (EU), zimepiga marufuku safari kutoka Uingereza, kufuatia kuzuka kwa virusi vipya vya corona. **PICHA/REUTERS**

# Mataifa yanusuru mkataba wa nyuklia na Iran

**Washington, MAREKANI**

MATAIFA yaliobakia katika mkataba wa nyuklia wa Iran wa mwaka 2015, yamesema yanajitayarisha kuikaribisha tena Marekani katika mkataba huo, chini ya utawala wa Joe Biden.

Katika mkutano wa mtandaoni, uliofanyika Jumatatu wa mawaziri wa mambo ya nje wa nchi zilizosaini mkataba wa nyuklia na Iran, walikubaliana kushughulikia uwezekano wa Marekani kurejea katika mkataba huo.

Nchi hizo ni pamoja na China, Urusi, Ujerumani, Ufaransa na Uingereza.

Katika mazungumzo hayo, Waziri wa Mambo ya kigeni wa Ujerumani, Heiko Mass, alisema mabadiliko ya utawala nchini Marekani, yanamaanisha Iran ina nafasi ya mwisho ya maendeleo ambayo haipaswi kupotezwa.

Alisema kwa sasa hawataraji kuona makubaliano yakikiukwa kama walivyoshuhudia hivi karibuni huku akionya kuwa hatua kama hizo huenda zikayumbisha zaidi makubaliano hayo ya nyuklia kati ya mataifa yalio na nguvu duniani pamoja na Iran. Mwenzake wa Uingereza, Dominic Raab, alisema katika mkutano huo, alikuwa wazi kabisa kuionya Iran kutotekeleza upanuzi ulioutangaza hivi karibuni wa mpango wake wa nyuklia.

Raab alisema hilo likifanyika, huenda likadidimiza maendeleo ya Iran, yaliotarajiwa kuonekana mwaka 2021.

Kwa upande wake, Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Iran, Mohammad Javad Zarif, aliahidi kupitia ujumbe wake wa twitter kwamba, taifa lake litabadili misimamo yake iliyochukua kufuatia Marekani kujiondoa katika mkataba wa nyuklia, iwapo mataifa yaliyosaini mkataba huo, yatasimamia majukumu yao ipasavyo.

Waziri Javad Zarif, alisema ni lazima watu wa Iran wahisi athari na utulivu wa kuondolewa kwa vikwazo vilivyolenga kuuharibu uchumi wake.

Licha ya Iran kukiuka masharti yaliyokubaliwa katika mkataba huo wa nyuklia wa mwaka 2015, shirika la nguvu za atomiki duniani IAEAy limeripoti kuwa Iran imeendelea kutoa idhini ya wachunguzi kufikia vinu vyake vya nyuklia ambayo ni makubaliano muhimu katika mkataba wa JCPOA.

Rais Mteule, Joe Biden atakayeingia rasmi madarakani Januari 20 mwakani, alidokeza kuwa Marekani itajiunga na mkataba huo unaofahamika kama mpango wa pamoja wa kuchukua hatua ama (JCPOA) ulionuiwa kuidhibiti dhamira ya Iran kujipatia silaha za nyuklia.

Mpango huo umekuwa ukiyumba tangu Rais Donald Trump alipoiondoa Marekani katika makubaliano ya nyuklia mwaka 2018 na kuiwekea Iran vikwazo zaidi vya kiuchumi.

Baada ya Marekani kujiondoa katika mkataba huo wa nyuklia, Iran imekuwa ikikiuka matakwa ya mkataba kwa kuongeza kiwango chake cha urutubishwaji wa madini ya urani katika shughuli zake za nyuklia.

Hivi karibuni Iran ilipanga kuongeza gesi ya urani kwenye mitambo ya kinu chake cha nyuklia, mpango uliokosolewa vikali na Ufaransa, Ujerumani na Uingereza.

***DW***

# Ripoti yabaini umaskini kupindukia Syria

**Damscus, SYRIA**

RIPOTI ya Benki ya Dunia na Shirika la Umoja wa Matiafa la kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), imesema madhara ya ugonjwa wa COVID-19 watu wanaokadiriwa kufikia milioni 4.4, ikiwamo wakimbizi milioni moja wa Syria na Wairaq wengine 180,000 waliokimbia makazi yao, wameanguka chini ya mstari wa umaskini.

Abdel Al Mahmoud, mkimbizi kutoka Syria anayeishi Lebanon aliyeanza kufanya kazi akiwa na umri wa miaka 12, baba yake alipoteza kazi kutokana na janga la COVID-19.

Abdel alilazimika kuihudumia familia nzima kwa kukusanya takataka ambazo zinatumika kuunda vitu vingine.

Abdel alisema, kulikuwa na kazi chache, hivyo akaamua kufanya kazi ya kulima, kwa kupanda ndimu.

"Kazi zilikuwa chache kabla ya virusi vya corona na sasa ni chache zaidi."

Familia ya kijana huyo, iliyakimbia makombora huko Syria mwaka 2013, wanaishi kwa msaada mdogo wa fedha wanaoupata kutoka UNHCR.

Ripoti hiyo ya Benki ya Dunia na UNHCR imeshauri kuwa mpango wa msaada wa fedha taslimu, unaosaidia kukabiliana na athari za corona, uongezwe kwa wakimbizi hao katika mwaka wa 2021.

***UN***

# Biden apewa chanjo ya Covid-19

**Washington, MAREKANI**

RAIS mteule wa Marekani, Joe Biden, amepatiwa chanjo dhidi ya virusi vya corona, wakati akitazamwa moja kwa moja kwenye televisheni, kutoa ushawishi kwa Wamarekani kuwa zoezi hilo ni salama.

Kabla ya kupokea chanjo hiyo, Biden alionekana akijiandaa na kisha kumweleza muuguzi kuendelea na shughuli wakati akiwa kwenye hospitali moja mjini Newark, Delaware.

Mkewe Jill Biden, saa kadhaa kabla, pia alipokea chanjo kwenye hospitali hiyo, ambayo iko karibu nyumbani kwao.

Baadhi ya viongozi wengine mashuhuri wa Marekani waliopokea chanjo hiyo ni pamoja na makamu wa rais Mike Pence, spika wa bunge, Nancy Pelosi na kiongozi wa walio wengi kwenye baraza la senata, Mitch McConnell.

Rais wa Marekani, Donald Trump ambaye, Oktoba alipatikana kuwa na virusi vya corona, kufikia sasa hajasema ni lini amepanga kuipokea.

Marekani inaongoza duniani kwenye idadi ya maambukizi huku tayari ikiwa imeshuhudia zaidi ya vifo 318,000 kutokana na Covid-19 kwa mujibu wa takwimu za Chuo Kikuu cha Johns Hopkins kilichopo Marekani.

***VOA***

# LAMPARD HANA HOFU UKAME KWA WENNER

**LONDON, England**

FRANK Lampard hana hofu na Timo Werner licha ya mshambuliaji huyo kuwa kwenye ukame wa kufunga mabao na kocha huyo wa Chelsea anaamini anaipambania timu.

Akiwa amesajiliwa kwa dau la pauni milioni 47.5 kutoka RB Leipzig kuelekea kuanza kwa msimu wa 2020-21, Werner amefunga mabao manne tu katika mechi 14 za Ligi Kuu England.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani ameshindwa kufunga katika mechi zote saba zilizopita kwenye mashindano yote kwa Chelsea, ukiwa ni muda mrefu zaidi tangu Septemba 2016 wakati akiwa akicheza kati ya Stuttgart na RB Leipzig.

Werner kwenye mchezo wa juzi Jumatatu ambao Chelsea ilishinda mabao 3-0 dhidi ya West Ham, alipiga mashuti manne na kutoa pasi moja ya mwisho kwa Tammy Abraham, na ingawa Lampard angependa bao kutoka kwa straika huyo, lakini alimtetea nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 kwa kushindwa kufunga.

"Sina shaka yoyote kwake. Kila mshambuliaji angependa kufunga mabao, kwani hilo ndilo jambo linalowahusu na ndio sababu Timo naye alitaka kupata mabao," alisema akiwaambia waandishi wa habari.


"Ni mchezaji ambaye yupo kwenye Ligi mpya na tunatakiwa kumpa nafasi, lakini anapata nafasi hiyo mara kwa mara, anazitisha timu na anazipa matatizo.

"Kwa sasa hayupo kwenye wakati mzuri, lakini muda huwa unabadilika, na ataendelea kupambana na tutaona mabao kutoka kwa Timo Werner kwa uhakika kabisa."

# LEWANDOWSKI AFUNGUKA KUTETA NA MANCHESTER UTD

**MUNICH, Ujerumani**

STRAIKA wa Bayern Munich, Robert Lewandowski, amebainisha alifanya mazungumzo na Alex Ferguson juu ya uhamisho wa kwenda Manchester United mwaka 2012.



Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland mara kwa mara alikuwa akihusishwa na kwenda Old Trafford wakati akiwa kule Borussia Dortmund, ambako alitumia misimu minne.

Hata hivyo, usajili wake ulishindwa kukamilika na badala yake akajiunga na wapizani wa Dortmund, Bayern kwa uhamisho huru mwaka 2014.

Amefunga mabao 266 katika mechi 307 alizoichezea Bayern na alikuwa mfungaji bora kwenye Bundesliga, DFB-Pokal na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, wakati 'Bavaria' hao wakibeba mataji matatu.

Lewandowski wiki iliyopita alitwaa tuzo ya mwanasoka bora wa kiume wa mwaka wa FIFA 2020, lakini amesema maisha yake ya soka yangekuwa tofauti kama BVB wasingezuia uhamisho wake wa kwenda Ligi Kuu England.

"Baada ya mwaka wa pili pale Dortmund, nilizungumza na Sir Alex Ferguson," alisema Lewandowski akiliambia jarida la France Football.

"Alinitaka mimi kwenda Manchester.

"Nilikuwa na nia. Naweza hata kucheza nilikuwa tayari. Lakini Dortmund hawakuwa tayari kuniachia niondoke."



# LAPORTA: NATAKA MESSI ABAKI BARCA

**BARCELONA, Hispania**

JOAN Laporta anataka Lionel Messi kubaki Barcelona na anaamini ana nafasi kubwa zaidi kuliko wagombea wengine wa urais wa klabu hiyo.

Messi mwenye umri wa miaka 33, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu, huku akiwa aliomba kuondoka Barca kabla ya kuanza kwa msimu huu wa 2020-21.

Awalia alikuwa rais kati ya mwaka 2003 na 2010, na sasa Laporta anawania tena kitu hicho na uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika Januari 24.


Laporta mwenye umri wa miaka 58, anataka Messi kubakia Barca na anahisi yeye ana nafasi kubwa ya kumbakiza kuliko mgombea mwingine yeyote.

"Kama nikishinda uchaguzi, nataka kuweka pendekezo la kishindani zaidi na najua atanisikiliza mimi. Nataka yeye abaki," alisema Laporta akiiambia RAC1.

"Nina nafasi kubwa kuliko wengine, anajua mara zote nilimtimizia kile nilichosema. Tuna mahusiano mazuri, tunaheshimiana kila mmoja.

"Kama nikiwa rais, nafikiri hilo litawezekana kirahisi zaidi kwangu kulifanikisha."

HABARI MICHEZO



# GUARDIOLA

## KUTOINGIA SOKONI DIRISHA JANUARI

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema hataingia sokoni katika dirisha dogo la Januari kwa ajili ya kutafuta mchezaji eneo la ushambuliaji licha ya madhaifu ya eneo hilo.

Mshambuliaji Sergio Aguero amekuwa na msimu mgumu hadi sasa kutokana na majeruhi, huku Gabriel Jesus alikosa mechi ya wikiendi iliyopita dhidi ya Southampton ambapo walishinda bao 1-0.

Pamoja na washambuliaji hao kukabiliwa na majeraha, Guardiola hataingia sokoni wakati wa dirisha dogo la Januari.


Usajili wa dirisha dogo kwa Uingereza litafunguliwa Januari 15, mwakani na Guardiola amesema hana mpango wa kumleta mshambuliaji.

"Hapana, sina mpango huo kwa sasa kutokana na hali ya uchumi na dunia ilivyokaa," alisema Guardiola baada ya kuulizwa na waandishi wa habari kama atafanya usajili Januari.

"Sasa kila klabu inapata shida, hatuwezi kukwepa hili".

## THURAM AFUNGIWA MECHI 6 KUMTEMEA MWENZAKE MATE

**DOTRMUND, Ujerumani**



STRAIKA wa Borussia Monchengladbach, Marcus Thuram amefungiwa mechi sita na Shirikisho la Soka la Ujerumani, DFB, kwa kumtemea mate, Stefan Posch wa Hoffenheim.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ameshapigwa panga la mshahara kwa tukio hilo na timu yake ya Gladbach alilolifanya kwenye mchezo huo wa kichapo cha mabao 2-1 katika dimba la Borussia-Park, Jumamosi.

Thuram alisisitiza kwamba hakuwa na nia ya kumtemea mate Posch na alimuomba radhi pamoja na Hoffenheim na wachezaji wenzake wa Gladbach, akisema atakubaliana na matokeo yoyote ya tukio hilo.

DFB ilithibitisha Jumatatu kwamba, Thuram ambaye ni mtoto wa nyota wa zamani wa Ufaransa, Lillian Thuram amefungiwa mechi tano za Ligi Kuu ya Bundesliga na DFB-Pokal, huku mechi ya sita ikipelekwa hadi Desemba 21, mwaka 2021.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Thuram, ambaye amefunga mabao manne kwenye mechi 20 katika mashindano yote kwa Gladbach msimu huu, pia amepigwa faini ya euro 40,000.

Akizungumzia tukio hilo, Mkurugenzi wa Michezo wa Gladbach, Max Eberl, alisema: "Nilikuwa na mazungumzo marefu na Marcus, ambapo aliomba radhi kwangu mimi na klabu kwa tukio lile.

"Tumemjua Marcus kwa karibia miaka miwili, tunaijua familia yake. Marcus alizidiwa na hasira ndio maana akamtemea mate Stefan Posch."



## JAMES WA UNITED AWANIWA BRIGHTON

**LONDON, England**

KLABU ya Brighton imeonyeshwa kuvutiwa na kiwango cha nyota wa Manchester United, Dan James na wanawania kutoa ofa ya kumsajili wakati wa dirisha dogo la Januari.

Kocha Mkuu wa Brighton, Graham Potter, anahitaji huduma ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 23, ili kuboresha kikosi chake ndani ya Ligi Kuu England ambayo imekuwa na ushindani mkubwa kwa msimu huu wa 2020/21.

Ripoti zinaeleza kwamba kiungo huyo ambaye alijiunga na Klabu ya Man United msimu wa 2019 kwa dau la pauni milioni 17, hajawa na nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Ole Gunnar Solkjaer na hajaonekana kwa muda wa miezi miwili kwenye kikosi jambo linalowapa nafasi Brighton kuipata saini yake.

Potter anaamini kuwa kutopata namba ndani ya kikosi hicho ni fursa kwake kumpata kiurahisi mchezaji huyo mwenye uwezo ndani ya uwanja kwa kuwa kikosi chake kinapambana kusaka ushindi.

Kwa msimu wa 2020/21, James amecheza jumla ya mechi tatu pekee za Ligi Kuu England, huku akionyeshwa kadi moja ya njano, United imecheza jumla ya mechi 12 na ina pointi 23 ikiwa nafasi ya saba.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA: WALA SIFIKIRII KUONDOKA ARSENAL

●●●Kama nikianza kusoma na kusikiliza kauli zote, ziwe chanya au hasi, zitaniendesha...

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema hana mpango wa kuachia kazi yake klabuni hapo na anahisi anasapoti yote ndani ya klabu hiyo.

'Washikabunduki' hao hawajashinda mechi yoyote kati ya saba zilizopita kwenye Ligi Kuu England, wakipoteza tano na kutoka sare mbili, wakiwa wametupwa nafasi ya 15 kwenye msimamo.

"Sitaki kufikiria kuhusu hatua hiyo (kuondoka) kwa sababu nitakuwa nafikiria kwa njia hasi na sitaki kufanya hivyo," alisema Arteta.

"Kwa wakati huu, natakiwa kujaribu hatua chanya zaidi kadri ninavyoweza."

Arteta alikuwa akizungumza kuelekea mchezo wa jana Jumanne wa Arsenal dhidi ya Manchester City wa robo fainali ya Kombe la Carabao.

"Tunapitia kipindi kigumu, kitu cha mwisho tunachotakiwa kufikiri ni kwamba, matatizo yetu yote yatamalizika kwa miezi michache ijayo. Sitaki kufikiria kuhusu matatizo kwa sasa," alisema.

"Najua majukumu niliyonayo na kwa nini nipo hapa. Kila mmoja anajua kwamba kutoka miezi michache iliyopita, haya mambo yasingeweza kumalizwa kirahisi na haraka. Nafikiri hilo ni jambo ambalo kila mmoja klabuni analijua."

Arteta aliteuliwa kuwa kocha wa Washikabunduki hao Desemba mwaka 2019 na ameiongoza klabu hiyo kushinda Kombe la FA na Ngao ya Jamii.

Hata hivyo, kikosi chake kimekuwa na wakati mgumu msimu huu na kimefunga mabao matatu katika mechi zake zaba za ugenini.

Alisisitiza kulikuwa na "umoja" kwenye vyumba vya kubadilishia nguo na ari ilikuwa "nzuri kama inavyotakiwa kuwa wakati wote tunapokuwa tunaumia kwa sababu ya matokeo ya Ligi Kuu na inatuumiza."

Raia huyo wa Hispania aliongeza kusema: "Kutoka kila kitu kilivyo klabuni hapa nahisi napata sapoti, hamasa na imani kubwa ambayo itatuwezesha kukipita kwa pamoja katika kipindi hiki kigumu.

"Ndani ya klabu tunastahili kupata vitu bora na kama mambo hayatokei hivyo, kila mmoja anakuwa na swali nini kinatokea.

"Mimi ndio mhusika namba moja linapokuja suala la matokeo, hivyo natakiwa kukubali hilo."

Arteta amesema hasikilizi "kauli zote" kuhusu klabu yake na amewataka wachezaji wake kufanya hivyo pia.

"Kama nikianza kusoma na kusikiliza kauli zote, ziwe chanya au hasi, zitaniendesha," alisema.

"Ushauri wangu ni kwa kila mchezaji kufanya hivyo hivyo. Kwenye mitandao ya kijamii wanaandika kila wanachokihisi na huwezi kuwazuia, hivyo ni hatari sana kama utasoma na kusikiliza kauli zote hizo." Alipoulizwa alikuwa anajisikiaje alipokuwa mchezaji timu ikiwa kwenye hali iliyonayo Arsenal kwa sasa, kiungo huyo wa zamani alijibu: "Nilikuwa napenda kujiangalia mimi, hata kama jambo lilikuwa linawahusu viongozi, makocha au wachezaji, nilitaka kuona wote tunakuwa na ari moja tu ya kupambana.

"Kwa kawaida mambo kama hayo yanapotokea, unakuwa na aina mbili ya watu: wapambanaji na waathirika.

"Unahitaji wapambanaji si waathirika. Waathirika huwa wanatafuta sababu. Waathirika wanaleta hisia hasi na wanaanza kulaumu kila kitu kinachotokea kwao au kama hakiendi sawa.

"Unahitaji watu wanaopambana, watu wenye mchango na ambao wapo tayari kufanya chochote kile kwa ajili ya kuipigania klabu kwa wakati kama huu."

## KWA UFUPI

**STONES MKATABA MPYA**

MLINZI wa Manchester City na England, John Stones mwenye umri wa miaka 26, anatarajiwa kuongezewa mkataba wa kuendelea kubaki pale Etihad baada ya kukubalika na kocha, Pep Guardiola msimu huu. ***(Telegraph)***

**ALABA AIKATALIA BAYERN**

MLINZI wa Bayern Munich na Austria, David Alaba, amekataa kusaini mkataba mpya na mabingwa hao wa Ulaya na anaweza kuzungumza na klabu mpya Januari. Chelsea, Real Madrid na Paris St-Germain zimeonyesha nia ya kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Mail)***

**GOMEZ AWANIWA ARSENAL**

ARSENAL ina nia ya kutaka kumsajili straika wa kimataifa wa Uruguay anayekipiga pale Valencia, Maxi Gomez mwenye umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

**DIGNE KUPEWA MKATABA**

EVERTON inaandaa mkataba mpya kwa mlinzi wake wa kushoto, Lucas Digne raia wa Ufaransa. Manchester City ni miongoni mwa klabu inayomwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Times)***

**NEWCASTLE, SHEFFIELD KWA ROJO**

NEWCASTLE United na Sheffield United zinawania kumsajili kwa mkopo mlinzi wa Manchester United na Argentina, Marcos Rojo mwenye umri wa miaka 30. ***(The Athletic)***

**PSG YAMWANIA OBLAK**

KLABU ya Paris St-Germain inapanga kutoa ofa kwa Atletico Madrid kwa ajili ya golikipa wake, Jan Oblak mwenye umri wa miaka 27, huku raia huyo wa Slovenia akiwa anataka changamoto mpya. ***(Mail)***

**JONES AWINDWA ENGLAND**

MLINZI wa Manchester United na England, Phil Jones mwenye umri wa miaka 28, anawaniwa kwa mkopo na West Bromwich Albion na Derby County. ***(Star)***

**CAICEDO ATAKIWA UNITED**

MANCHESTER United inataka kumsajili kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 19, kutoka Independiente del Valle wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Manchester Evening News)***

**GUARDIOLA KUTOSAJILI JANUARI**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola hatarajii kusajili wachezaji wapya wakati wa dirisha dogo la Januari, licha ya Gabriel Jesus na Sergio Aguero wote waukosa mchezo wa ushindi wa 1-0 dhidi ya Southampton, Jumamosi. ***(Goal)***

**WILLIAMS AGOMEWA LIVER**

MLINZI wa Liverpool na timu ya Taifa ya Vijana ya England chini ya umri wa miaka 21, Rhys Williams mwenye miaka 19, hataruhusiwa kuondoka kwa mkopo. Alikuwa anawaniwa na klabu za ligi za chini ikiwamo Middlesbrough. ***(Sun)***

**SAM AMTISHA LIVERMORE**

KOCHA mpya wa West Brom, Sam Allardyce, amemshutumu kiungo Muingereza, Jake Livermore na kudokeza kwamba nyota huyo mwenye umri wa miaka 31, anaweza kupoteza unahodha wake baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu wakati wakifungwa na Aston Villa mabao 3-0 Jumapili. ***(Independent)***

HABARI MICHEZO

# NAMUNGO YAAHIDI KUMALIZA KAZI KWA WASUDAN CHAMAZI

**Na Saada Akida**

WAKATI wakishuka dimbani leo kuikaribisha Al Hilal Obayed ya Sudan, wawakilishi wa Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika, Namungo FC, wamesema mipango yao ni kumaliza kazi katika mechi hiyo ya nyumbani kwa kuhakikisha wanapata ushindi mkubwa dhidi ya wapinzani wao hao.

Namungo ambayo imetinga hatua hiyo ya raundi ya kwanza baada ya kuitoa Al Rabita FC ya Sudan Kusini kwa jumla ya mabao 3-0, itawakaribisha wageni wao hao katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam majira ya saa 11 jioni.

Timu hizo zitarudiana kati ya Januari 5-6, mwakani na mshindi wa jumla atasubiri kupangiwa mechi moja ya mchujo nyumbani na ugenini dhidi ya timu zitakazotolewa raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa na mshindi wa jumla atakuwa amefuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Tayari kikosi cha Namungo kimerejea jijini Dar es Salaam tangu jana kikitokea visiwani Zanzibar ambapo kiliweka kambi kujiandaa na mchezo huo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, alisema wachezaji wake wako fiti na tayari kwa ajili ya mchezo huo utakaopigwa leo jioni.

Alisema mechi hiyo ni muhimu sana kwao kupata matokeo kwa kuhakikisha wanatumia vema uwanja wa nyumbani kushinda kwa idadi kubwa ya mabao ili kumaliza kazi.

"Tumejipanga vizuri, na wachezaji wako fiti tayari kwa mechi hiyo, tunahitaji kumaliza mechi yetu nyumbani kwa kutafuta idadi kubwa ya mabao ili tukienda kwao tusicheze kwa presha kubwa.

"Nimefanikiwa kuangalia video za mechi zao na kubaini wanapenda kucheza na kumiliki mpira na wenzetu ni warefu hasa katika safu ya ulinzi, tumefanyia kazi upungufu wetu sasa tunaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri," alisema Morocco ambaye amerithi mikoba hiyo kutoka kwa Mnyarwanda Thierry Hitimana aliyeibukia Mtibwa Sugar ya Morogoro baada ya kuachana na miamba hiyo ya Ruangwa mkoani Lindi.

NIPO VIZURI...




Kipa namba mbili wa Simba, Beno Kakolanya, akiwa mazoezini Harare nchini Zimbabwe, kujiandaa na mechi ya kwanza ya hatua ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum itakayopigwa leo katika Uwanja wa Taifa wa Zimbabwe. Kakolanya anatarajiwa kubeba jahazi la timu hiyo langoni kutokana na Aishi Manula kuwa majeruhi. **PICHA: SIMBA**

# Hitimana kuanza na straika Simba Mtibwa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu mpya wa Mtibwa Sugar, Mnyarwanda Thiery Hitimana, ambaye leo ataiongoza timu hiyo kwa mara ya kwanza tangu ajiunge nayo wiki iliyopita, amependekeza jina la mshambuliaji wa Simba, Charles Ilanfya, kuwa miongoni mwa nyota anaowataka kukiongezea nguvu kikosi hicho kwenye usajili huu wa dirisha dogo.

Hitimana ambaye amejiunga na timu hiyo baada ya kuachana na Namungo FC, leo ataiongoza timu hiyo wakati itakapoikaribisha Dodoma Jiji FC kwenye mechi yao ya kukamilisha mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana, ambaye ameipokea timu hiyo ikiwa katika nafasi ya saba na alama zake 22 kwenye msimamo wa ligi hiyo, alisema amebakiza nafasi moja ya mshambuliaji wa kusajili kipindi hiki cha dirisha dogo na amempendekeza nyota huyo wa Simba ambaye amesikia taarifa kuwa kuna uwezekano akatolewa kwa mkopo.

Alisema tayari uongozi wake unafanyia kazi mapendekezo yake ya kupata huduma ya Ilanfya, ambaye amekuwa akitakiwa kwa mkopo na timu nyingi ikiwamo Ihefu FC.

"Niliwaomba nisajili wachezaji watatu, ila nimeona kuna nyota kutoka kikosi cha vijana wa timu hiyo wanafanya vizuri, hivyo nikaomba wazungumze na Simba ili tupate huduma ya Ilanfya.

"Nimeona safu ya ushambuliaji ni tatizo kubwa, hivyo tukimpata Ilanfya kuja kuongeza nguvu na waliokuwapo ndani ya timu, nina uhakika wakupata matokeo mazuri zaidi," alisema Hitimana.

Alisema Ilanfya ni mchezaji nzuri, hivyo ana imani akipata huduma ya nyota huyo atafanya vizuri kwa sababu anafahamu ubora wake mbele ya lango tangu msimu uliopita. Alisema malengo yake ni kurejesha heshima na ubora wa timu hiyo kama ilivyokuwa zamani hadi kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi.

"Mwongozo wa timu ni kurudi katika ubora wao, kuhakikisha tunatafuta pointi tatu, ili kutoka katika nafasi za chini, tunahitaji hadi mzunguko wa pili tusiwe na presha ya kutaka kujinusuru kushuka daraja bali tuwe tunapambania kutafuta namba sita za juu ya msimamo," alisema Hitimana.

## Black Sailor yataka tatu za Zimamoto

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MZUNGUKO wa tano wa Ligi Kuu Zanzibar unatarajiwa kuanza leo kwa kupigwa michezo mitatu katika viwanja tofauti visiwani hapa, mechi zote zikipigwa majira ya saa kumi alasiri.

Katika Uwanja wa Amaan, timu ya Kipanga itaumana na KVZ FC, huku kwenye Dimba la Mao A timu ya Black Sailor ikivaana na Zimamoto, wakati Uwanja wa Gombani Kisiwani Pemba, timu ya Hard Rock itakuwa nyumbani kuwakaribisha Maafande wa Polisi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Black Sailor, Juma Awadhi, alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa kuwa anacheza na timu ambayo inauzoefu wa muda mrefu katika ligi hiyo.

Alisema wamejipanga kuhakikisha hawapotezi mchezo huo licha ya ukweli kwamba utakuwa mgumu kwa upande wao, lakini anaamini lolote linaweza kutokea uwanjani.

"Wachezaji wangu wapo vizuri na wamejipanga kuhakikisha tunapata alama tatu, mpaka sasa timu inaendelea na maandalizi ya mchezo huo, kikubwa ni wachezaji kuhakikisha hawatoki mchezoni," alisema.

Black Sailor inashirikia nafasi ya sita katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama saba baada ya kushuka dimbani mara tano huku wapinzani wao katika mechi ya leo, Zimamoto wakiwa nafasi ya nne na pointi nane.

## Mayungu aiokoa Gwambina usiku

**Na Mwandishi Wetu**

BAO la usiku (dakika za majeruhi) kupitia kwa Japhet Mayungu, limeikosesha Mbeya City ushindi dhidi ya wenyeji wao, Gwambina FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa jana kwenye uwanja wa Gwambina uliopo Misungwi nje kidogo ya Jiji la Mwanza.

Katika mechi hiyo ambayo Mbeya City ilitangulia kupata bao kipindi cha kwanza dakika ya 35 kupitia kwa straika Kibu Prosper, Gwambia ilipigana kiume kwa muda wote hadi iliposawazisha dakika za majeruhi.

Kwa matokeo hayo, mechi hiyo iliyopigwa majira saa nane mchana, Mbeya City iliendelea kushika nafasi ya pili kutoka mkiani ikiwa na alama zake 13, mbili mbele ya Mwadui FC iliyokuwa ikiburuza mkia kabla ya mchezo wao wa jana dhidi ya Coastal Union uliopigwa majira saa 10 alasiri.

Gwambina yenyewe ipo nafasi ya 11 ikiwa na pointi 19 baada ya mechi 16, hivyo inaweza kupanda zaidi endepo itashinda mechi yake ya mwisho ya mzunguko wa kwanza.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena leo kwa kupigwa michezo mitatu ambapo JKT Tanzania itakuwa mwenyeji wa KMC FC huku Ihefu FC ikiwaalika vinara wa ligi hiyo, Yanga katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na Mtibwa Sugar ikiwakaribisha Dodoma Jiji FC.

# Michezo

Jumatano Desemba 23, 2020

Nipashe




## ARTETA: WALA SIFIKIRII KUONDOKA ARSENAL

HABARI UK 22

### TUPO TAYARI...



Wachezaji wa Simba, beki Pascal Wawa ( jezi namba 6 ) na straika Chris Mugalu wakiwa mazoezini Harare, Zimbabwe, kujiandaa na mechi ya kwanza ya raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum itakayopigwa katika Uwanja wa Taifa wa Zimbabwe leo. **PICHA: SIMBA**

# SVEN: BOCCO, MANULA 'OUT', HAKUNA NAMNA

●●●Asema wataikosa FC Platinum leo, lakini Wawa, Nyoni wasema ushindi haukwepeki...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya nyota wao wawili waliosafiri na kikosi hadi nchini Zimbabwe kutarajiwa kuikosa mechi dhidi ya wenyeji wao, FC Platinum, mabingwa wa soka wa Tanzania, Simba wamesema wanachokitaka leo ni ushindi tu katika mchezo wao wa kwanza wa raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba itashuka katika Uwanja wa Taifa wa Zimbabwe leo kuvaana na FC Platinum kusaka nafasi ya kufuzu hatua ya makundi ya michuano hiyo, huku ikiwakosa nahodha na mshambuliaji tegemeo, John Bocco pamoja na kipa namba moja, Aishi Manula, imeelezwa.

Juzi Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, aliliambia Nipashe kuwa Bocco na Manula walisafiri wakiwa majeruhi na walikuwa wakiendelea na matibabu nchini humo kuona kama wanaweza kucheza leo, lakini jana Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, alisema wamejaribu kila kitu ili wawe tayari kwa mchezo huo ila itakuwa ngumu.

"Tuna saa chache kabla ya mchezo, tumejaribu kila kitu ili wawe tayari kwa mchezo, lakini itakuwa ngumu kuwa tayari [John Bocco] bado yuko kitandani hayuko sawa, Aishi [Manula] aliumia mchezo uliopita na anaweza kuchukua wiki zaidi ili kuwa sawa, mpaka sasa kuna uwezekano asilimia 50 ya kuwapo kwenye mchezo," alisema Sven.

Lakini pamoja na kutarajia kuwakosa nyota hao, wachezaji wenzao wameahidi kupambana kufa kupona kuhakikisha wanarejea nchini na ushindi ili kurahisisha kazi katika mechi ya marudiano itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam Januari 6, mwakani.

Beki wa kati, Erasto Nyoni akizungumza baada ya mazoezi ya jana asubuhi, alisema mchezo huo wanauchukulia kwa umakini mkubwa sana na anaamini kocha Sven kawafuatilia vizuri wapinzani wao, hivyo kinachotakiwa ni kuwaombea tu waamke salama leo ili kuweza kusaka ushindi.

"Platinum ni timu moja nzuri, ninaimani kocha kaifuatilia vizuri na imani yangu ni kwamba tukiamka salama tunaweza kufanya vizuri, binafsi nimejiandaa vizuri kukabiliana na hawa Platinum, lakini kikubwa tumejiandaa kama timu kwa sababu mchezo wa mpira ni mchezo wa kutegemeana.

"Kwa mtu mmoja mmoja katika kichwa ama akili, ila kila mmoja anaiangalia mechi hiyo na kuiwaza kwa sababu Simba kuna wachezaji wengi na wazoefu, pia tuna uzoefu na mashindano haya, kikubwa ni kila mmoja 'kuswichi' akili yake," Nyoni alisema.

"Sisi tupo kwa ajili ya kuiwakilisha nchi na hatupo kwa ajili ya Simba pekee, ila tupo kwa nembo ya Simba, kikubwa naomba wananchi na Wanasimba wote kutuombea ili tuweze kufanya vizuri."

Wakati Nyoni akishuka na mistari hiyo, beki mwenzake wa kati, Pascal Wawa yeye alisema: Wote tunajua nini tunachokita na tunajua kwa nini tupo hapa Zimbabwe, tunataka kushinda, tunataka kufanya vizuri, tunataka kufika mbali katika mashindano haya na hilo linabaki kuwa lengo letu katika michuano hii."

"Tayari tumepita kizingiti kimoja na sasa tunakabiliana na kingine, ambacho kinaonekana kuwa kigumu, lakini kwa namna yoyote ile tutakaposhuka dimbani, tutafanya kile tunachotakiwa kukifanya; kushinda mechi kwa ajili yetu na nchi."

Simba ambayo imetinga hatua hiyo baada ya kuitoa Plateau ya Nigeria kwa bao 1-0, endapo itaitoa FC Platinum itafuzu moja kwa moja hatua ya makundi ya michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

FC Platinum yenyewe ilitinga hatua hiyo kwa kuitoa Costa do Sol ya Msumbiji kwa jumla ya mabao 4-1, ikishinda 2-1 ugenini na kuhitimisha kwa ushindi wa mabao 2-0 nyumbani.

# `NTIBAZONKIZA MBELEKO YA YANGA KWA IHEFU LEO?

**Na Mwandishi Wetu**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga leo wanashuka dimbani kuhitimisha raundi ya kwanza ya ligi hiyo, huku wakiwa na morali mpya baada ya usajili wao wa dirisha dogo, Mrundi Saidi Ntibazonkiza, kuanza kwa fungua akaunti yake ya mabao katika timu hiyo.

Yanga ambayo ipo kileleni ikiwa na pointi 40, katika mechi iliyopita dhidi ya Dodoma Jiji, ilimchezesha Ntibazonkiza kipindi cha pili akitokea benchi kuchukua nafasi ya Michael Sarpong wakati huo matokeo yakiwa 1-1, ambapo alifunga bao la pili na kuhusika kwenye la tatu lililofungwa na beki Bakari Mwamnyeto akiunganisha nyavuni mpira wa faulo ndogo iliyopigwa na straika huyo.

Ntibazonkiza anaonekana kuwa mkombozi kwa safu ya ushambuliaji ya Yanga kutokana na uwezo wake mkubwa wa kutoa pasi za mwisho na kufunga, hivyo ni mchezaji ambaye safu ya ulinzi ya Ihefu FC leo inapaswa kuwa makini naye.

Hata hivyo, itashuka katika Uwanja wa Sokoine kuivaa Ihefu ambayo ipo nafasi tatu kutoka mkiani na pointi zake 13, lakini nayo ikiwa na kumbukumbu nzuri ya ushindi wa bao 1-0 iliyoupata uwanjani hapo kwenye mechi iliyopita dhidi ya KMC FC.

Kocha wa Yanga, Cedric Kaze, amesema anatambua hakuna mchezo rahisi katika ligi hiyo, lakini anaimani kikosi chake kitafanya vizuri kwenye mechi hiyo itakayopigwa leo majira ya saa 10 alasiri.

Alisema lengo lao ni kuona wanamaliza raundi ya kwanza kwa kushinda ili kuendelea kujizatiti kileleni mwa ligi hiyo ambayo msimu huu inashirikisha timu 18.

"Wachezaji wapo tayari kwa mchezo huu, na kila mmoja anatambua tunatakiwa kupata matokeo ili kuendelea kuongoza kwenye msimamo," alisema.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002